# KATIBA MPYA
# INAYOPENDEKEZWA

**TOLEO JEPESI**

KATIBA Institute
Constitution as an Instrument of Change

## YALIYOMO

*Ukurasa*


Dibaji ..... 2

Utangulizi ..... 3

Sura ya Kwanza: Mamlaka ya Wananchi na Ukuu wa Katiba ..... 4

Sura ya Pili: Jamhuri ..... 5

Sura ya Tatu: Maadili ya Taifa, Kanuni na Malengo ..... 6

Sura ya Nne: Uraia ..... 7

Sura ya Tano: Utamaduni ..... 8

Sura ya Sita: Sheria ya Haki za Binadamu ..... 8

Sura ya Saba: Ardhi na Mali ..... 15

Sura ya Nane: Mazingira na Maliasili ..... 17

Sura ya Tisa: Uongozi na Uaminifu ..... 19

Sura ya Kumi: Uwakilishi wa Watu ..... 21

Sura ya Kumi na Moja: Bunge ..... 25

Sura ya Kumi na Mbili: Mamlaka ya Utendaji ..... 33

Sura ya Kumi na Tatu: Mahakama ..... 43

Sura ya Kumi na Nne: Serikali ya Wilaya ..... 48

Sura ya Kumi na Tano: Fedha za Umma na Usimamizi wa Mapato ..... 53

Sura ya Kumi na Sita: Huduma kwa Umma ..... 57

Sura ya Kumi na Saba: Usalama wa Taifa ..... 59

Sura ya Kumi na Nane: Tume za Kikatiba ..... 64

Sura ya Kumi na Tisa: Marekebisho ya Katiba ..... 66

Sura ya Ishirini: Masharti ya Kijumla ..... 67

Sura ya Ishirini na Moja: Masharti ya Akiba, Mpito na Yanayotokana na Kuidhinishwa kwa Katiba Hii ..... 69


KATIBA Institute
Constitution as an Instrument of Change

## DIBAJI

Toleo hili jepesi la Katiba Mpya Inayopendekezwa limetayarishwa na Tume ya Kurekebisha Katiba ya Kenya kufuatana na maagizo ya sheria ya kurekebisha Katiba ya Kenya kwa jumla, na hasa Kifungu 17 cha Sheria hiyo.

Kifungu 17(a) kinaipatia Tume uwezo "wa kutoa na kuwezesha elimu ya raia ili kuhimiza mazungumzo na ufahamu wa masuala ya Kikatiba miongoni mwa wananchi." Kifungu 17(e) hasa kinaipatia Tume uwezo "wa kutoa na kuwezesha elimu ya raia ili kufanikisha Kura ya Maoni."

Kijitabu hiki kinatarajiwa kuwa toleo la muhtasari na rahisi kuelewa la Katiba Mpya Iliyopendekezwa na kuchapishwa na Mwanasheria Mkuu mnamo Agosti 22, 2005. Kijitabu hiki kinaonyesha masharti muhimu katika Katiba Mpya Inayopendekezwa na kinayarahisisha ili yaweze kueleweka na Wakenya wote.

Kijitabu hiki hakikusudiwi kuchukua nafasi ya Katiba Mpya Inayopendekezwa. Katiba Mpya Inayopendekezwa ni waraka rasmi wenye sifa za kisheria. Ikiwa pana mgongano baina ya waraka huu na Katiba Mpya Inayopendekezwa kama ilivyochapishwa, ifahamike kwamba Katiba Mpya Iliyopendekezwa ndiyo itakayofuatwa kwa sababu ndio waraka rasmi wenye sifa za kisheria. Kwa hivyo, Tume inawahimiza Wakenya wote wasome Katiba Mpya Inayopendekezwa kama ilivyochapishwa na Mwanasheria Mkuu.

Tume ingependa kutambua na kutoa shukrani kwa Makamishna wafuatao waliokuwa wanachama wa Jopo lililotayarisha kijitabu hiki kabla hakijaidhinishwa na Tume katika mkutano wa pamoja: Prof. Wanjiku Kabira, Naibu Mwenyekiti wa Tume na Mjumuishi wa Jopo; Dkt. K. Musonik Arap Korir, Mjumuishi wa Jopo; Bi. Abida Ali-Aroni, Mwenyekiti wa Tume; Prof. H.W.O. Okoth-Ogendo, Mwenyekiti wa Kamati Saidizi ya Utafiti, Urasimu na Utaalamu; Bi. Kavetsa Adagala; Bw. John Mutakha Kangu; Bw. Ahmed Issack Hassan; Bw. Paul Musili Wambua; na Bi. Salome Wairimu Muigai.

Tume pia ingependa kutambua na kutoa shukrani kwa Maafisa wa Tume walioshiriki katika kutayarisha kijitabu hiki: Bi. Pauline Nyamweya, Naibu Katibu; Bw. Harrison Ndoria Gicheru; Bw. Jeremiah Nyegenye; Bi. Eunice Gichangi; Bi. Selina Achieng Olende; na Bi. Noor Awadh Ghalgan.

KATIBA Institute
Constitution as an Instrument of Change

# UTANGULIZI

**Sehemu hii inahusu yale tunayotangaza kwenye Katiba, pamoja na:**
- **Nani anatengeneza Katiba?**
- **Kwa nini inatengenezwa?**
- **Inasemaje hasa?**

***Utangulizi ni nini?***

Utangulizi hueleza ni nani anayetengeneza Katiba na kwa nini inatengenezwa, pamoja na mambo mengine.




KATIBA Institute

*__Utangulizi wetu unasemaje?__*

Katika utangulizi, tunasherehekea historia ya nchi yetu kama taifa moja. Tunafurahia uanuwai wa jamii zetu, tamaduni na dini. Tunaweka malengo tunayokusudia kuyafikia kama taifa. Tunatambua Mungu na tunamwomba aibariki nchi yetu.


## SURA YA KWANZA: MAMLAKA YA WANANCHI NA UKUU WA KATIBA

**Sura hii inahusu:**

- **Kutoa maamuzi**
- **Kudhibiti mambo yetu**
- **Sheria zetu**

*__Mamlaka ya Wananchi ni Nini?__*

Uwezo wa kukata kauli na kudhibiti mambo yote yanayohusu nchi uko nasi, watu wa Kenya. Tunautekeleza uwezo huu kupitia wawakilishi tuliowachagua na vyombo mbalimbali vya taifa vilivyoundwa na Katiba. Vyombo hivi ni: Bunge, Mamlaka ya Nchi, Mahakama na Tume za Kikatiba katika viwango vyote na afisi za taifa.




KATIBA Institute

*__Ni sheria zipi zinazotawala nchi yetu?__*

Sheria kuu na muhimu zaidi nchini mwetu ni Katiba. Sheria nyingine ni pamoja na sheria zilizotungwa na Bunge, sheria za binafsi zinazotegemea mila, tamaduni au dini, sheria za Jumuiya ya Afrika Mashariki na sheria zinazohusika za kimataifa.

***Ukuu wa Katiba ni nini?***

Hii ina maana kwamba Serikali na kila mtu nchini Kenya ni sharti atii Katiba. Hakuna mtu anayeweza kupinga uhalali wa Katiba. Kama Mkenya una wajibu wa kuheshimu na kutetea Katiba yetu. Kila mtu nchini Kenya sharti atii Katiba yetu.

## SURA YA PILI: JAMHURI

**Sura hii inahusu:**
- **Nchi yetu**
- **Serikali yetu**
- **Lugha zetu**
- **Sikukuu zetu**
- **Dini zetu**

Kenya ni Jamhuri na ni nchi huru. Eneo la Kenya limegawanywa katika wilaya na viwango vingine kama itakavyoagizwa na sheria. Tunatekeleza utukufu wetu wa kujitawala katika ngazi mbili za Serikali, zitakazoshirikiana kwa manufaa yetu. Ngazi hizi ni ngazi ya taifa na ngazi ya wilaya.



Mji mkuu wa Kenya ni Nairobi.

Lugha ya taifa ni Kiswahili.

Lugha rasmi ni Kiswahili na Kiingereza.

Alama za taifa la Kenya zimo katika Jedwali ya Kwanza ya Katiba, na kuonyeshwa hapa nchini.

KATIBA Institute Constitution as an Instrument of Change

| | | |
|---|---|---|
|  |  |  |
| *Bendera ya Taifa* | *Nembo* | *Muhuri wa Kenya* |

***Siku za Kitaifa ni zipi?***

Siku ya kitaifa ni siku ambayo tunasherehekea matukio muhimu katika historia ya nchi yetu. Sikukuu za kitaifa ni –

| | |
|---|---|
| Juni 1: | Sikukuu ya Madaraka; |
| Oktoba 20: | Sikukuu ya Mashujaa; |
| Disemba 12: | Sikukuu ya Jamhuri. |

***Ni nini uhusiano baina ya taifa na dini?***

Masuala ya dini na masuala ya taifa lazima yatenganishwe. Hakuna dini ya taifa na dini zote zitachukuliwa kwa usawa.

## SURA YA TATU: MAADILI YA TAIFA, KANUNI NA MALENGO


**Sura hii inahusu:**


- **Yanayotuongoza tunapofafanua Katiba**

Maadili ya taifa, kanuni na malengo yanakusudiwa kuongoza vyombo vya taifa na kutuongoza tunapotumia au kufafanua Katiba. Ni pamoja na:

- umoja wa nchi yetu;
- uwazi wa serikali na maafisa wake;
- kuchukua hatua kumaliza ufisadi;
- kuhakikisha kushiriki kikamilifu kwa wanawake, watu wenye ulemavu, jamii zilizotengwa na raia wengine wote katika maisha ya nchi; na hasa, kutekeleza kanuni ya kwamba hakutakuwa na zaidi ya thuluthi mbili za watu wa jinsia moja katika mashirika ya kuteuliwa au kuchaguliwa;
- kusimamia maliasili za taifa letu kwa manufaa ya watu wote wa Kenya; na
- kulinda mazingira ili yatunufaishe sasa na pia vizazi vitakavyokuja baada yetu.

KATIBA Institute
Constitution as an Instrument of Change



# SURA YA NNE: URAIA

**Sura hii inahusu:**

- **Hadhi yetu kama raia**
- **Wajibu wetu kama raia**

***Raia wa Kenya ni nani?***

Wewe ni raia wa Kenya ikiwa ulipozaliwa baba au mama yako alikuwa raia wa Kenya.

Mtu asiye raia anaweza kuomba na anaweza kusajiliwa kama raia ikiwa amefunga ndoa na raia wa Kenya kwa kipindi kisichopungua miaka saba.

Mtu asiye raia na ambaye ni mkaazi wa Kenya kwa kipindi kisichopungua miaka saba mfululizo, anaweza kuomba kusajiliwa kama raia wa Kenya.

Mtu asiye raia anaruhusiwa kuishi Kenya kama ilivyoidhinishwa na sheria.

Mtoto anayepatikana Kenya mwenye chini ya miaka minane, na ambaye utaifa wake haujulikani, atachukuliwa kuwa raia wa Kenya.




KATIBA institute
Constitution as an Instrument of Change

***Unaweza kuwa raia wa Kenya na wa nchi nyingine?***

Raia wa Kenya anaweza kuwa raia wa nchi nyingine bila kupoteza uraia wake. Raia wa nchi nyingine anaweza pia kuomba kuwa raia wa Kenya.

Raia wa Kenya ana haki ya kupewa paspoti na hati yoyote ile ya utambulisho.

***Ni nini wajibu wa raia wa Kenya?***

Raia ana wajibu wa:

- kuelewa, kutii na kulinda Katiba na sheria nyinginezo;
- kupiga kura;
- kufanya kazi ili kujikimu binafsi na familia yake na kuendeleza maslahi ya jamii;
- kulipa kodi;


- kulinda mazingira;
- kujiepusha na vitendo vya ufisadi; na
- kuendeleza demokrasia na utawala bora.

## SURA YA TANO: UTAMADUNI

**Sura hii inahusu:**
- ❖ **Kuheshimu na kulinda tamaduni zetu**

***Utamaduni katika Katiba***

Tamaduni mbalimbali, mila, maadili, desturi, historia, dini, dawa, hadithi, na njia za mavazi zinatambuliwa na zinatufanya tujivunie kuwa Wakenya. Tunahitajika kuzielewa na kuzilinda. Ni lazima pia tuwasaidie watoto wetu na watu wengine kujifunza tamaduni zetu.




***Tume ya Kitaifa ya Utamaduni***

Tume hii ndiyo chombo maalum cha Taifa katika kulinda na kuendeleza utamaduni. Hushauri kuhusu mambo yote ya sera ya utamaduni.

***Siku ya Utamaduni***

Tunasherehekea tamaduni zetu pamoja kama Wakenya kila Disemba 26. Hii ni Sikukuu ya Utamaduni.

## SURA YA SITA: SHERIA ZA HAKI ZA BINADAMU

**Sura hii inahusu:**
- ❖ **Haki zetu kama binadamu**

***Sheria ya Haki za Binadamu ni Nini?***

Kila binadamu ana haki fulani ambayo ni muhimu sana. Haki hizi zinaitwa haki za binadamu. Kuheshimu na kulinda haki hizi ni muhimu ili kila mtu na kila jamii iheshimiwe.

KATIBA Institute Constitution as an Instrument of Change

Haki hizi hazitolewi na Serikali na Serikali pia haiwezi kuziondoa. Serikali ina wajibu wa kutambua, kuheshimu na kulinda haki hizi.

***Haki za Binadamu ni za nani?***

Haki za binadamu ni za kila mtu. Pia zinahusu Serikali na vyombo vyake na maafisa wake wanapofanya kazi. Wanatarajiwa kuheshimu na kulinda haki za binadamu. Wanatakikana pia kujua namna ya kushughulikia mahitaji maalum ya watu binafsi na makundi tofauti ya jamii. Isitoshe, serikali inahitajika kutekeleza mikataba ya kimataifa ya haki za binadamu iliyoidhinisha.

***Mtu anaweza kulalamika wapi kuhusu kunyimwa haki za binadamu?***

Ikiwa umenyimwa haki zako au mtu ametisha kukunyima haki zako, una haki ya kulalamikia mahakama au Tume ya Haki za Binadamu na Haki za Kiutawala. Mahakama inaweza kutangaza kuwa umenyimwa haki zako na kuamuru ulipwe fidia. Inaweza pia kuamuru kwamba hatua iliyochukuliwa na mtu fulani si halali.

***Je, kuna kanuni za kunufaika haki?***

Sheria inaweza kuweka kanuni za mipaka ya haki. Hii ni muhimu ili kunufaika haki zako kusiwanyime wengine haki zao. Lakini kanuni sharti ziwe za haki na zinazokubalika kidemokrasia.

***Haki ya kuishi na usawa***



Haki mojawapo ni haki ya kuishi. Tangu mtu akiwa tumboni mwa mamake, yeye ni mtu na ana haki ya kuishi. Kutoa mimba hakuruhusiwi isipokuwa katika hali fulani kama ilivyoidhinishwa na Sheria ya Bunge.


Una haki ya kutendewa sawa na wengine na kutobaguliwa kwa sababu ya rangi, jinsia, dini, hali ya afya au sababu nyingine.

***Wanawake na wanaume wana haki gani?***

Wanawake na wanaume wana haki sawa katika masuala yote pamoja na kuwa na mali au kurithi. Hakuna sheria, utamaduni au mila itakayokuwa halali ikiwa inawanyima wanawake au wanaume haki zao.

***Haki ya wazee katika jamii***

Wazee katika jamii ni watu wenye umri wa miaka sitini na zaidi. Wanaendelea kuwa na haki kamili na serikali sharti iwasaidie na iwalinde.




***Haki za vijana***

Serikali sharti ichukue hatua na ianzishe miradi ya kuwanufaisha vijana. Sharti iwasaidie vijana kupata elimu, mafunzo na ajira na isaidie kushiriki kwao katika masuala ya umma.

***Haki za watoto***

Watoto wana hadhi maalum katika jamii. Ni jukumu la familia na serikali kuwaelimisha na kuwalinda.

Watoto wote, iwe wamezaliwa ndani au nje ya ndoa, wana haki sawa. Maslahi ya mtoto ni muhimu zaidi katika kila jambo linalohusu mtoto. Mama na baba mtoto wana haki sawa na jukumu sawa katika kulinda na kuyakidhi mahitaji ya mtoto. Kila mtoto ana haki zifuatazo, pamoja na zingine –



- ya kupata chakula, malazi, na huduma za afya;
- ya kupata elimu ya msingi, bila malipo na ya lazima;
- ya kulindwa kutokana na madhara yoyote;
- ya kutokamatwa au kutiwa kizuizuini isipokuwa kama kufanya hivyo ni hatua ya mwisho; na
- pale ambapo mtoto ametiwa nguvuni au kizuizini atenganishwe na watu wazima na apewe wakili na serikali.

KATIBA Institute
Constitution as an Instrument of Change

***Familia***

Familia ni uti wa mgongo wa taratibu za kijamii.

***Haki za kuoa/kuolewa***

Kila mtu ana haki ya kuoa au kuolewa na mtu wa jinsia tofauti ikiwa wamekubaliana na wote wana umri wa miaka kumi na minane au zaidi. Mke na mume wana haki sawa katika ndoa. Bunge litatunga sheria inayotambua ndoa zilizotimizwa chini ya mila au taratibu tofauti za kidini.

***Haki za watu wenye ulemavu zimelindwa?***

Watu wenye ulemavu wana haki sawa na watu wasiokuwa na ulemavu. Pia wana haki ya kupewa heshima. Serikali itatunga sheria kuhakikisha watu wenye ulemavu wananufaika kutokana na haki zao.

***Kuzuiliwa utumwa, mateso na kukamatwa kinyume na sheria***

Hakuna mtu anayeruhusiwa kumtesa mwingine au kumfanya mtumwa.

***Haki ya dini***

Una haki ya kuwa mfuasi wa dini yoyote au kutofuata dini, na kuitekeleza. Hakuna mtu aliyeruhusiwa kumlazimisha mwingine kuamini dini au kuitekeleza. Pia mtu hawezi kunyimwa ajira au huduma nyinginezo kwa ajili ya dini.

KATIBA Institute
Constitution as an Instrument of Change

***Haki ya kutoa maoni na kupata habari***

Kila mtu ana haki ya kutoa maoni na kupata habari muhimu zilizoko mikononi mwa serikali. Vyombo vya habari kama vile magazeti, televisheni, redio au vinginevyo vina haki ya kufanya kazi kwa uhuru bila kuingiliwa na serikali.

***Uhuru wa kushirikiana***

Una uhuru wa kukutana na kushirikiana na wengine na kuunda mashirika. Unaweza pia kuunda au kujiunga na chama cha kisiasa au cha wafanyakazi.

***Uhuru wa kwenda utakako***

Una haki ya kwenda utakako nchini Kenya. Pia una haki ya kuondoka nchini.

***Wakimbizi***

Mkimbizi ana haki ya kukaa Kenya ikiwa maisha yake yatahatarishwa akiondoka nchini.

***Nina haki ya kuchagua kazi? Na wafanyakazi wana haki zipi?***

Una uhuru wa kuchagua kazi au biashara. Wafanyakazi wana haki ya kutendewa haki, kufanya kazi katika hali nzuri, na kupewa malipo ya haki. Wana haki ya kujiunga na chama cha wafanyakazi wakipendacho na pia kugoma.

***Kuwa na mali***

Una haki ya kuwa na mali. Bunge haliruhusiwi kutunga sheria inayoruhusu serikali kuchukua mali hiyo bila sababu ya kutosha. Serikali inaweza kuchukua mali ya mtu kwa manufaa ya umma na sharti ilipe fidia kabla ya kufanya hivyo.

***Haki nyingine***


Kila Mkenya ana haki ya –

- kupewa ruzuku na serikali ikiwa hawezi kujiruzuku au familia yake;
- huduma ya afya;
- elimu;
- makaazi;
- chakula;
- maji;
- usafi;
- mazingira safi na salama;
- lugha na utamaduni; na
- kulindwa kama mteja wa bidhaa au huduma.

Serikali sharti itunge sheria ili kuhakikisha kuwa haki hizi zinatekelezwa kwa muda ufaao.

***Ni nini haki za watu waliotiwa nguvuni?***

Kila mtu aliyetiwa nguvuni sharti afahamishwe mara moja sababu ya kutiwa nguvuni na aruhusiwe kuzungumza na wakili au mtu yeyote anayeweza kumsaidia. Hakuna mtu atakayemlazimisha mwingine kukiri au kukubali kwamba amefanya uhalifu.




Mtu aliyetiwa nguvuni lazima afikishwe mbele ya mahakama haraka iwezekanavyo lakini isiwe baada ya saa arobaini na nane tangu alipokamatwa. Mtu ana haki ya kuachiliwa kwa kuweka rehani au dhamana kabla ya kufanyiwa mashtaka, isipokuwa kuwe na sababu inayolazimisha iwe vinginevyo. Ikiwa hatia inaweza kuadhibiwa kwa kutoza faini au kifungo cha chini ya miezi sita, mshtakiwa hatawekwa rumande.

KATIBA Institute
Constitution as an Instrument of Change

***Kufanyiwa kesi ya haki***

Kila mtuhumiwa ana haki ya kufanyiwa mashtaka ya haki yanayojumuisha –

- kuchukuliwa kutokuwa na hatia hadi ithibitishwe kuwa ana hatia;
- kufahamishwa shtaka na kupewa muda wa kutosha na pamoja na vifaa ili ajitayarishe kujitetea;
- mashtaka kuanzishwa na kukamilishwa bila kucheleweshwa kusikokuwa na sababu ya kutosha;
- kuwakilishwa na wakili aliyemchagua au anayelipwa na Serikali, ikiwa yaonekana hatatendewa haki asipokuwa na wakili; na
- kukata rufani.

***Haki ya mtu aliye kizuizini***

Mtu aliyewekwa kizuizini ataendelea kuwa na haki zake za kimsingi chini ya Katiba, isipokuwa haki hiyo iwe haiambatani na madhumuni ya kuwa kizuizini.

***Kutangazwa Hali ya Hatari***

Hali ya Hatari inaweza tu kutangazwa ikiwa nchi:

- imevamiwa na nchi nyingine;
- imetishiwa kivita au na maafa ya kimaumbile; au
- imekabiliwa na hali nyingine za dharura za kitaifa.

Wakati kuna Hali ya Hatari huenda tusinufaike na haki zetu zilizoko kwenye Sheria ya Haki za Binadamu. Hali ya Hatari isizidi muda wa siku kumi na nne, isipokuwa kama Bunge litaamua kuongeza muda wa tangazo.

Mahakama Kuu inaweza kuamua uhalali wa kutangazwa Hali ya Hatari au hatua zilizochukuliwa chini yake. Sheria yoyote iliyotungwa kufuatia tangazo la Hali ya Hatari inaweza kukiuka Sheria ya Haki za Binadamu endapo tu kukiuka huko kunahitajika na Hali hiyo ya Hatari. Sheria hiyo inayokiuka Haki za Binadamu sharti iambatane na sheria ya kimataifa inayohusiana na Hali ya Hatari.

***Tume ya Haki za Binadamu***

Kuna Tume mbili zilizoundwa ili kusaidia Taifa kutekeleza kanuni za Sheria ya Haki za Binadamu.

Tume hizi ni:

- Tume ya Jinsia; na
- Tume ya Haki za Binadamu na Haki za kiutawala.

Tume ya Jinsia ina wajibu wa kuendeleza usawa miongoni mwa wanaume na wanawake katika masuala yote ya maendeleo ya nchi. Pia inashauri Serikali kuhusu mambo yote yanayohusu jinsia na maendeleo.

Tume ya Haki za Binadamu na Haki za kiutawala ina wajibu hasa wa kulinda na kuendeleza haki za binadamu nchini.

KATIBA Institute
Constitution as an Instrument of Change

## SURA YA SABA:   ARDHI NA MALI

**Sura hii inahusu:**
- **Ardhi na Mali yetu**

Ardhi ni rasilmali kuu ya nchi yetu.  Na pia ni mali ya watu wote wa Kenya na msingi wa maisha yao.  Ardhi sharti ihifadhiwe na itumiwe kwa njia ambayo ni adilifu, ya kufaa na ya usawa.

***Sera za serikali kuhusu ardhi***

Sera ya ardhi itakayotengenezwa na serikali lazima ihakikishe kuwa –

- kuna usawa wa kupata ardhi kwa wananchi wote;
- watu wanatumia ardhi kwa hali yenye manufaa na uzalishaji;
- kuna ulinzi wa haki za ardhi kwa wote wanaomiliki ardhi;
- ardhi inatumika kwa njia inayohifadhi na kulinda mazingira;
- wanawake na wanaume hawabaguliwi katika kumiliki na kutumia ardhi; na
- ikiwezekana, usuluhishaji wa mizozo ya ardhi ufanywe katika ngazi ya mashinani.


KATIBA Institute
Constitution as an Instrument of Change




**Kuna ardhi za aina gani?**

Kuna aina tatu za ardhi.  Hizi ni:

- ardhi ya umma;
- ardhi ya jamii; na
- ardhi ya binafsi




***Ardhi ya umma ni ipi?***

Ardhi ya umma ni ardhi ambayo iko mikononi mwa serikali au chombo cha umma. Hii ni pamoja na misitu ya serikali, barabara, mbuga na hifadhi za wanyama, mito, maziwa na bahari. Ardhi ya umma haiwezi kuuzwa au kutolewa isipokuwa kwa mujibu wa sheria.

***Ardhi ya jamii ni ipi?***

Hii ni ardhi ambayo iko mikononi mwa jamii maalum na ni pamoja na maeneo ya kulisha mifugo, mahala pa ibada na ardhi ya jadi iliyokaliwa kitamaduni na jamii za wawindaji na wakusanyaji. Pia haiwezi kuuzwa au kutolewa isipokuwa kwa mujibu wa sheria.

***Ardhi ya binafsi ni ipi?***

Hii ni ardhi ambayo si ya umma na si ya jamii. Ni ardhi inayomilikiwa na mtu au watu. Umilikaji huo unaweza kuwa wa daima au wa muda maalum.

***Wageni wanaweza kumiliki ardhi?***

Hapana. Mtu ambaye si raia wa Kenya hawezi kumiliki ardhi nchini Kenya. Lakini mtu huyo anaweza kukodisha ardhi. Ukodishaji huo hautazidi miaka tisini na tisa. Mtu asiye raia anaweza kumiliki ardhi tu kwa njia ya kukodisha.

KATIBA Institute
Constitution as an Instrument of Change

***Udhibiti wa matumizi ya ardhi***

Serikali ina uwezo wa kudhibiti matumizi ya ardhi yoyote. Serikali itatumia uwezo wake wa namna ardhi itatumiwa kwa njia yenye manufaa kwa umma.

***Sheria za Ardhi***

Bunge litatunga sheria kuhakikisha matumizi bora ya ardhi kwa manufaa ya watu wetu.

***Tume ya Kitaifa ya Ardhi***

Tume hii itasimamia masuala yote ya ardhi na kazi yake ni pamoja na:-

- kusimamia ardhi yote ya umma;
- kushauri serikali kuhusu sera ya ardhi;
- kuchunguza mizozo ya umilikaji wa ardhi na kusaidia kuisuluhisha; na
- kusaidia katika kubadilisha sheria na sera za ardhi.

***Afisi za Tume ya Kitaifa ya Ardhi iko wapi?***

Tume ya Kitaifa ya Ardhi itaanzisha afisi kote nchini.

## SURA YA NANE: MAZINGIRA NA MALIASILI

**Sura hii inahusu:**

- ❖ **Mazingira yetu**
- ❖ **Maliasili yetu**

***Ni nini wajibu wa Serikali kuhusu mazingira na maliasili?***

Serikali lazima ilinde na ihifadhi mazingira na maliasili yetu. Wajibu wake ni –

- kuhakikisha kuwa mazingira yametumiwa vyema;
- kuzuia kuchafuliwa na kuharibiwa kwa mazingira;
- kuendeleza uhifadhi wa nishati na matumizi ya kudumisha vyanzo vya nishati;
- kuendeleza upandaji miti ili angalau asilimia kumi ya eneo la ardhi ya Kenya iwe na miti; na
- kuhakikisha kuwa faida itokanayo na maliasili na mazingira inagawanywa kwa uadilifu na inatumiwa kwa manufaa ya Wakenya.

***Ni nini wajibu wa mwananchi kuhusu mazingira na maliasili?***

Wajibu wetu kuhusu mazingira ni –

- kutumia maliasili kwa kuwajibika;
- kulinda na kuheshimu mazingira;
- kutofanya kitendo kinachoharibu mazingira;
- kuhakikisha mazingira safi, salama na yenye afya; na
- kutoa taarifa kwa serikali kila unapoona kitendo kinachoharibu mazingira.




***Nifanye nini kuhakikisha tuna mazingira safi na yenye afya?***

Una haki ya kuwa na mazingira safi na yenye afya. Ikiwa mazingira si safi na haidumishi afya, unaweza kwenda mahakamani.

***Tume ya Kitaifa ya Mazingira***

Kazi ya Tume hii ni –

- kushauri serikali kuhusu njia bora za kutumia mazingira;
- kuhakikisha kuwa mazingira yamelindwa na yametumiwa kwa kuwajibika na uadilifu; na
- kuhakikisha kuwa mipango na miradi ya Serikali kuhusu mazingira inatekelezwa.

KATIBA Institute
Constitution as an Instrument of Change

***Sheria kuhusu mazingira***

Bunge litatunga sheria kuhakikisha matumizi bora ya mazingira.



# SURA YA TISA: UONGOZI NA UAMINIFU

**Sura hii inahusu:**

- **Tabia zetu tukiwa uongozini**

Ukuu wa kuamua na kudhibiti mambo yote yanayohusu nchi ni yetu sisi, Wakenya. Ukuu huu wetu wa kujitawala mara nyingine huenda ukatekelezwa kwa niaba yetu na maafisa wa Serikali. Afisa wa Serikali ni mtu aliyeshikilia mamlaka ya afisi iliyoanzishwa na Katiba hii. Maafisa wote wa umma ni maafisa wa Serikali. Afisa wa Serikali sharti –

- atii Katiba;
- aheshimu watu waliompa uwezo wa kutawala;
- aheshimu afisi anamofanyia kazi; na
- ale kiapo au tamko la dhati kabla ya kuchukua mamlaka ya afisi yake.

***Maafisa wa Serikali wawe na nidhamu***

Afisa wa serikali atakuwa anafuata masharti iwe ni katika mwenendo wa hadharani na kirasmi au katika Maisha ya kibinafsi. Masharti haya ni pamoja na –

- maafisa wa Serikali watakuwa wamehitimu na wanaoweza kutekeleza wajibu wao;
- maamuzi ya maafisa wa Serikali yawe yenye uadilifu na yasiyopendelea; na
- maafisa wa Serikali wawe na nidhamu na wajitolee kazini.

KATIBA Institute Constitution as an Instrument of Change

Pamoja na hayo, Afisa wa Serikali –

- hatatumia afisi ya Serikali kwa maslahi ya kibinafsi;
- hataomba au kukubali rushwa;
- hatatumia vibaya pesa za umma;
- hatatumia uwezo wa afisi yake kunyanyasa kijinsia au kimwili mtu yeyote; na
- hataamuru mtu mwingine kufanya kitendo kisicho halali.

Ikiwa afisa wa Serikali amehukumiwa kwa hatia inayohusiana na masuala haya, afisa huyo ataachishwa kazi na hatapewa kazi nyingine katika afisi yoyote ya Serikali.




***Kutangaza mali***

Afisa wa Serikali atawasilisha taarifa ya maandishi au matangazo kwa Tume ya Maadili na Uaminifu. Taarifa itataja mali na madeni yake. Pia itataja rasilmali na madeni ya Afisa wa Serikali, ya mkewe au mumewe, na ya watoto wa Afisa wa Serikali ambao hawajaoa au kuolewa na ambao hawajafikisha umri wa miaka kumi na minane. Taarifa hizi zitawasilishwa-

- mara tu akiwa afisa wa Serikali;
- kila mwaka Wakati akiwa afisa wa Serikali;
- akiacha kuwa afisa wa Serikali.

KATIBA Institute
Constitution as an Instrument of Change

***Je, afisa wa Serikali anaweza kuwa na akaunti ya benki nje ya Kenya?***

Afisa wa Serikali hawezi kuwa na akaunti ya benki nje ya Kenya isipokuwa iruhusiwe na sheria.

***Na je kuhusu zawadi au msaada kwa afisa wa Serikali?***

Zawadi au msaada kwa afisa wa serikali katika shughuli ya umma au rasmi si ya afisa huyo na sharti itolewe kwa Serikali.




***Je, Afisa wa Serikali anaweza kuwa na kazi nyingine yenye mshahara?***

Afisa wa Serikali aliyeajiriwa kwa kazi ya kudumu hatafanya kazi nyingine yenye mshahara.

***Sheria kuhusu uongozi***

Bunge litatunga sheria kuendeleza na kutekeleza uongozi bora na uaminifu.

***Tume ya Maadili ya Uaminifu***

Tume ya Maadili ya Uaminifu ndiyo yenye wajibu wa kutekeleza maadili na uaminifu miongoni mwa maafisa wa Serikali. Baadhi ya majukumu ya Tume ya Maadili na Uaminifu ni –

- kupokea taarifa au matangazo ya maafisa wa serikali;
- kuwezesha ukaguzi wa taarifa au matangazo hayo kwa yeyote;
- kupokea malalamiko kutoka kwa watu kuhusu mienendo ya maafisa wa serikali; na
- kusaidia katika kuzuia ufisadi.

KATIBA Institute
Constitution as an Instrument of Change

## SURA YA KUMI: UWAKILISHI WA WATU

**Sura hii inahusu:**
- **Kuwakilisha Wakenya katika kuhudumia umma**

***Kanuni za uchaguzi***

Katiba yetu ina kanuni za jumla kama ifuatavyo –

- raia wote wanaostahiki wana haki ya kupiga kura au kugombea uchaguzi;

- upigaji kura katika uchaguzi utakuwa kwa kura ya siri;
- upigaji kura katika uchaguzi utakuwa huru na haki;
- uchaguzi utahakikisha uwakilishaji sawa wa wanaume na wanawake, na vikundi vilivyotengwa; na
- uchaguzi utaendeshwa na chombo huru ambacho kitalindwa dhidi ya kuingiliwa.

***Sheria za Uchaguzi***

Bunge litatunga sheria kuhusu –

(a) idadi na ukubwa wa maeneo ya uchaguzi kwa ajili ya uchaguzi wa Bunge;

(b) utaratibu wa uteuzi wa wagombea uchaguzi;

(c) utaratibu wa upigaji kura;

(d) usajili wa kuendelea wa raia kama wapiga kura;

(e) usimamizi wa uchaguzi na kura ya maamuzi;


(f) usajili wa, na kupiga kura kwa raia waishio nje ya Kenya.

KATIBA Institute
Constitution as an Instrument of Change

***Kupiga Kura***

Katika kila uchaguzi, Tume ya uchaguzi na mipaka itahakikisha kwamba-

- utaratibu wa upigaji kura ni mwepesi;
- sanduku la kura litakalotumiwa litakuwa lenye kuonyesha;
- kura zilizopigwa zitahesabiwa na kutangazwa kwenye kituo cha kupigia kura;
- mipango maalum imefanywa ili wapiga kura wote waweze kupiga kura, pamoja na Wakenya wanaoishi ng'ambo, wafungwa, vikosi vya ulinzi wa Kenya, na wagonjwa mahospitalini;



- hatua zimechukuliwa kuhakikisha kuwa uchaguzi ni huru na haki.

***Ni nani awezaye kupiga kura?***

- Unaweza kupiga kura kama wewe ni raia na una umri wa miaka kumi na minane au zaidi.

- Raia anaweza kusajiliwa kama mpiga kura katika kituo kimoja tu cha usajili.
- Mipango ya usajili sharti iruhusu raia wote waliohitimu kupiga kura au kugombea uchaguzi.

***Wagombea wa kujitegemea***

Mgombea wa kujitegemea ni mgombea uchaguzi ambaye hajateuliwa na chama chochote katika uchaguzi wa Bunge au kiti cha serikali ya wilaya.

Una haki ya kusimama kama mgombea wa kujitegemea ikiwa –

- wewe ni raia wa Kenya;
- hujakuwa mwanachama wa chama cha kisiasa kilichosajiliwa kwa muda wa miezi sita kabla ya tarehe ya uchaguzi unaogombea;
- umesajiliwa na Tume ya Uchaguzi na Mipaka kama mgombea wa kujitegemea;
- umetimiza masharti ya kanuni za maadili kwa wagombea wa kujitegemea yaliyotayarishwa na Tume ya Uchaguzi na Mipaka;
- umeteuliwa na idadi ifuatayo ya wapiga kura waliosajiliwa katika eneo la uchaguzi ambapo unataka kugombea-
  (i) ikiwa ni kiti cha Bunge, wapiga kura elfu moja (1000); na
  (ii) ikiwa ni kiti cha wilaya, wapiga kura mia tano (500).

KATIBA Institute
Constitution as an Instrument of Change

***Wagombea bila kupingwa***

Ikiwa kufikia mwisho wa siku za uteuzi ni mgombea mmoja tu aliyeteuliwa, mgombea huyo atatangazwa mshindi.

***Uwakilishi katika mashirika ya kimataifa***


Kwa kufuatana na mikataba inayohusika, Bunge litatunga sheria itakayoongoza uteuzi na uchaguzi wa wawakilishi wa Kenya katika vyombo vya kisheria vya Kimataifa.

***Tume ya Uchaguzi na Mipaka***

Tume ya uchaguzi na mipaka ina wajibu wa:-

- usajili unaoendelea wa wapiga kura;
- kuunda na kuweka mipaka ya maeneo ya uchaguzi;
- kuhakikisha kuwa uchaguzi ni huru, haki na umesimamiwa inavyopasa;
- kusimamia vyama vya kisiasa;

- kusuluhisha mizozo midogo wakati wa uchaguzi;
- kuelimisha raia kuhusu namna ya kutekeleza haki ya kupiga kura na kukubali demokrasia kama njia ya kuishi;
- kuwachuja wagombea wa viti vya Rais, Bunge na Serikali za wilaya kwa kushauriana na Tume ya Maadili na Uaminifu; na
- kuweka, kuchunguza na kubadilisha mipaka ya utawala ya wilaya na ngazi nyinginezo.





***Mipaka ya maeneo ya uchaguzi na utawala***

Tume ya Uchaguzi na Mipaka ndiyo inayoamua majina na mipaka ya maeneo ya uchaguzi na utawala. Katika kufanya hivyo, Tume ni sharti –

- ishauriane na watu na makundi ya watu walioathiriwa;
- ihakikishe kuwa maeneo yote ya uchaguzi yana idadi karibu sawa; na
- kuhusu kila eneo la uchaguzi izingatie:
    (i) uhusiano wa jamii zilizoko;
    (ii) idadi ya watu na mikondo ya ongezeko;
    (iii) sifa za kujiografia;
    (iv) njia za mawasiliano;
    (v) mipaka iliyopo ya maeneo ya utawala.

Tume sharti ichunguze majina na mipaka ya maeneo ya uchaguzi kila baada ya kipindi kisichozidi miaka kumi.

KATIBA Institute
Constitution as an Instrument of Change




***Vyama vya Kisiasa***

Vyama vya kisiasa vina nafasi muhimu katika uchaguzi. Kabla uchaguzi haujafanywa, vyama vya kisiasa hufanya kampeni za uchaguzi na huteua wagombeaji. Chama kinachoshinda au kikundi cha vyama huunda serikali. Katiba imetoa masharti ya kimsingi yanayopasa kufuatwa na vyama vyote vya kisiasa.

***Masharti ya kimsingi ya vyama vya kisiasa***

Chama cha kisiasa lazima kiwe na sura ya kitaifa. Hii ina maana kwamba chama cha kisiasa hakiwezi kuwa na msingi, kwa mfano, wa kabila, eneo, rangi, jinsia au dini. Chama cha kisiasa sharti kiendeleze maadili, kanuni na malengo ya taifa na utawala wa kisheria.

KATIBA Institute
Constitution as an Instrument of Change

Chama cha kisiasa hakina budi –

- kutii kanuni za demokrasia katika shughuli zake na kiwe na uongozi uliochaguliwa kidemokrasia;
- kuendeleza na kudumisha umoja wa taifa;
- kuendeleza na kuheshimu haki za binadamu; na
- kuzingatia kanuni za maadili ya vyama vya kisiasa.

Sheria ya Bunge imeeleza kuhusu usimamizi wa vyama vya kisiasa, pamoja na –

- wajibu wa majukumu;
- usajili, usimamizi na nidhamu; na
- uhasibu na ukaguzi.

## SURA YA KUMI NA MOJA: BUNGE

**Sura hii inahusu:**
- **Kazi za wale wanaotunga sheria**
- **Namna wanavyopata na kupoteza kazi zao**

Nchini Kenya, ngazi ya juu ya utungaji sheria ni Bunge. Majukumu yake ni –

- kutunga sheria;
- kuhakikisha uadilifu katika kugawa maliasili;
- kuidhinisha uteuzi wa baadhi ya maafisa wa serikali;
- kuchunguza tabia ya Rais, Naibu Rais na maafisa wengine wa Serikali;
- kuchukua hatua ya kuwafuta kazi maafisa hawa, ikibidi; na
- kutafakari na kuidhinisha mikataba ya kimataifa.

***Ni nani wabunge?***

Bunge lina –

- wajumbe waliochaguliwa kutoka maeneobunge na idadi yao imewekwa na sheria;
- wanawake waliochaguliwa kutoka maeneo maalum yaliyowekwa na sheria;
- wanachama walioteuliwa na vyama vya kisiasa;
- Mwanasheria Mkuu
- spika; na
- mawaziri walioteuliwa kutoka nje ya Bunge.

KATIBA Institute Constitution as an Instrument of Change

Miongoni mwa wabunge walioteuliwa na vyama vya kisiasa –


- asilimia tano ya wabunge wote ni watu wenye ulemavu na thuluthi moja ni wanawake;
- asilimia tano ya wabunge wote wanawakilisha makundi yenye maslahi maalum, pamoja na vijana na wafanyakazi;
- wabunge kadha wanateuliwa ikiwa wanaume au wanawake hawakufikia angalau thuluthi moja ya wabunge wote.

Mwanasheria Mkuu, Spika au Mawaziri walioteuliwa nje ya Bunge ni wabunge kwa sababu tu ya nafasi zao na kwa muda ule ambapo wameshikilia nyadhifa hizo. Hawapigi kura kuhusu suala lolote Bungeni.

*Ni nani anayeweza kuwa mbunge?*

Mtu anaweza kuwa mbunge, ikiwa mtu huyo –

- ni raia;
- ni mpiga kura wa eneobunge lolote aliyesajiliwa;
- ametimiza kiwango cha elimu au uadilifu kilichowekwa na sheria;
- ameteuliwe na chama cha kisiasa;
- ni mgombea wa kujitegemea ambaye lazima aungwe mkono na wapiga kura elfu moja au zaidi.




*Ni nani asiyeweza kuwa mbunge?*

Mtu hawezi kuwa mbunge ikiwa mtu huyo –

- ameshikilia afisi ya umma, lakini si mbunge;
- hana akili timamu;
- ni muflisi (amefisilika na imetangazwa hivyo) na hajasamehewa;
- anatumikia kifungo kisichopungua miezi sita;
- alikuwa, kwa muda wowote katika kipindi cha miaka kumi iliyopita, akitumikia hukumu ya kifungo isiyopungua miaka mitatu;
- ameondolewa katika afisi ya umma kwa sababu ya utovu mkubwa wa nidhamu;
- amepatikana kuwa alitumia vibaya afisi ya umma.

*Uchaguzi wa wabunge hufanywa lini?*

Uchaguzi wa wabunge lazima ufanywe siku ya Jumanne.  Siku ya uchaguzi ni Jumanne inayotangulia siku ishirini na nane kabla ya muhula wa Bunge kumalizika.

KATIBA Institute Constitution as an Instrument of Change

Uchaguzi mdogo utafanywa kabla ya siku tisini kumalizika baada ya nafasi ya ubunge kutokea. Lakini ikiwa siku zilizobakia kabla ya uchaguzi si zaidi ya siku tisini basi uchaguzi mdogo hautafanywa. Ikiwa nafasi ni ya mbunge ambaye hakuchaguliwa moja kwa moja, basi mkutano wa uchaguzi unaohusika utateua mtu mwingine kabla ya siku arobaini na mbili kumalizika.

***Nafasi ya mbunge kuwa wazi***

Mtu atakoma kuwa mbunge –

- akijiuzulu kwa kumwandikia Spika taarifa;
- ikiwa mtu huyo hastahiki kuwa mbunge;
- ikiwa Bunge limemaliza muda wake;
- ikiwa mbunge hakuhudhuria vikao vinane bila ruhusa ya maandishi kutoka kwa Spika na bila sababu ya kutosha;
- ikiwa mbunge ameondolewa kwa kuvunja kanuni zinazohusu uongozi na uadilifu wa maafisa wa Serikali;
- ikiwa mbunge amejiunga na chama cha kisiasa ijapokuwa aliingia Bunge kama mgombea wa kujitegemea; au
- ikiwa mbunge amekihama chama chake cha kisiasa kilichomteua alipokuwa mgombea uchaguzi.

KATIBA Institute
Constitution as an Instrument of Change

***Kutatokea nini ikiwa kuna swali kuhusu uchaguzi au uteuzi wa mbunge ama kuhusu nafasi ya ubunge?***

Mahakama Kuu sharti itoe kauli kabla miezi sita haijamalizika.

***Kutatokea nini kama chama kikivunjwa au vyama vikiungana?***

Mbunge hatachukuliwa kwamba amejiuzulu chamani ikiwa chama kilichomteua –

(i) kimevunjwa;

(ii) muungano ambamo chama chake kimo umevunjwa; au

(iii) chama chake kimeungana na vyama vingine.

***Utaratibu wa kutunga sheria***

Kutunga sheria kunaanza na Mswada. Mswada una mapendekezo ya sheria mpya au mabadiliko ya sheria iliyopo.

Mswada unaweza kuwasilishwa Bungeni na mbunge yeyote. Miswada ya fedha inaweza kuwasilishwa na Waziri pekee. Miswada ya fedha inahusu kukusanya na kutumia fedha za umma.

Kabla Mswada haujakuwa sheria hupitia hatua mbalimbali. Ikiwa Mswada umepitishwa, hupelekewa Rais ili auidhinishe. Rais anaweza kuidhinisha au arudishe Mswada pamoja na mapendekezo. Ikiwa Bunge, baada ya kutilia maanani maoni ya Rais, litapitisha Mswada kwa mara ya pili, Mswada utarudishiwa Rais ili aidhinishe.

Rais ataidhinisha na Mswada utakuwa sheria. Mswada utachapishwa kwenye Gazeti la Serikali kama Sheria ya Bunge. Lakini Rais akikataa kuidhinisha, Mswada utakuwa sheria bila idhini ya Rais.

***Mswada huanza kutumikaje kama Sheria ya Bunge?***

Mswada ambao umepitishwa na Bunge na kuidhinishwa na Rais –

- huchapishwa kwenye Gazeti ndani ya siku saba tangu uidhinishwe;
- utaanza kutumika baada ya siku saba tangu uchapishwe kwenye Gazeti.

Lakini, ikiwa sheria iliyochapishwa kwenye Gazeti –

- imetaja tarehe ambayo itaanza kutumika, hiyo ndiyo tarehe itakapoanza kutumika;
- imewapa Wabunge maslahi ya kifedha moja kwa moja (kama mishahara na marupurupu), itaanza kutekelezwa baada ya Bunge lililoipitisha kuvunjwa.

***Ninaweza kupata wapi sheria zilizotungwa?***

Kuna masjala ya umma iitwayo Masjala ya Sheria inayohifadhi sheria zote zilizopitishwa na Bunge, na pia sheria zilizopitishwa na wajumbe wa wilaya. Sheria hizo zinapatikana kwa –

- Kiswahili;
- Kiingereza; na
- Breli.

Nakala ya sheria iliyoidhinishwa na Bunge na wajumbe wa wilaya itapatikana katika maktaba zote za umma.

***Bunge hukaa wapi?***

Makao ya Bunge yako Nairobi.  Lakini –

- Rais anaweza kuchagua mahali pengine kwa kikao cha kwanza cha Bunge;
- ikihitajika, Bunge linaweza kukaa mahali pengine.

***Ni sheria zipi zinazoongoza Bunge?***

Bunge hutunga kanuni kwa utekelezaji wa kazi zake.  Kanuni hizi huitwa Kanuni za Bunge.

***Kamati za Bunge***

Bunge lina kamati zinazosaidia katika kutekeleza majukumu.  Kamati ina uwezo wa kumwita mtu yeyote ili asaidie katika utekelezaji wa majukumu yake.

***Kufanya kazi na kukutana Bungeni***

Bunge sharti litekeleze majukumu yake kwa uwazi.  Lazima lifanye mikutano yake na ya kamati zake mbele ya watu.  Hii inaruhusu umma kushiriki katika kazi ya Bunge. Unaruhusiwa kuhudhuria Bunge ila tu pawe na sababu maalum ya wewe kutoruhusiwa.

***Je, nina haki ya kulalamikia Bunge?***

Kila mtu ana haki ya kulalamikia Bunge ili kutunga, kubadilisha au kufuta sheria yoyote.




***Akidi ya Bunge ni ipi?***

Akidi ya Bunge ni asilimia thelathini ya wabunge wote.

***Lugha rasmi za Bunge ni zipi?***

Lugha rasmi za Bunge ni Kiswahili, Kiingereza na lughaishara.

***Maamuzi yanatolewa vipi Bungeni?***

Jambo lolote lililoletwa Bunge linatolewa maamuzi kwa kupigiwa kura na idadi kubwa zaidi ya wabunge waliopo na waliopiga kura.  Lakini kuna wakati Katiba inahitaji wingi tofauti wa kura.

KATIBA Institute Constitution as an Instrument of Change

Ikiwa idadi ya wanaopinga na wanaounga mkono ni sare, jambo linalopigiwa kura haliidhinishwi.

Mbunge haruhusiwi kupiga kura kuhusu jambo ambalo ana maslahi ya kifedha ya moja kwa moja. Mbunge akipiga kura kwa jambo hilo, kura yake itapotea.

***Uwezo, haki na kinga kwa Bunge na wabunge***

Wabunge wana uhuru wa kuzungumza na kujadili Bungeni. Hawawezi kuhojiwa au kushtakiwa katika mahakama yoyote kwa yale waliyosema au kufanya Bungeni wakati walitekeleza wajibu wao. Lakini lazima watii Kanuni za Bunge na wanaweza kuadhibiwa na Bunge wasipotii.

***Maafisa wa Bunge***

Maafisa wa Bunge ni wa makundi mawili –

- Maafisa ambao ni wabunge – yaani, Spika na Naibu Spika; na
- Maafisa wasiokuwa wabunge. Maafisa hawa wanatoa huduma za kiutawala na kitaalamu Bungeni.

***Spika na Naibu Spika huchaguliwa vipi?***

Spika huchaguliwa na Bunge kutoka miongoni mwa watu ambao si wabunge lakini wana sifa zinazohitajika kwa wabunge. Naibu Spika anachaguliwa kutoka miongoni mwa wabunge.

***Kazi ya Spika na Naibu Spika ni ipi?***

Spika na Naibu Spika wanasimamia Bunge na kuhakikisha kuwa Kanuni za Bunge zinafuatwa. Ndio wanaoongea kwa niaba ya Bunge kwa jumla katika uhusiano wake na watu wasio wabunge.

***Karani wa Bunge***

Karani anachaguliwa na Tume ya Huduma ya Bunge kwa kuidhinishwa na Bunge.

Karani –

- anaajiriwa kwa utaratibu wa kudumu na mapato ya uzeeni;
- anastaafu akitimiza miaka sitini na tano;

KATIBA Institute Constitution as an Instrument of Change

- anaweza kuondolewa madarakani kwa kura iliyoungwa mkono na asilimia sitini na tano ya wabunge au zaidi.

***Kiongozi wa Upinzani***

Kiongozi wa Upinzani ni mbunge aliyechaguliwa na chama kikubwa zaidi au muungano wa vyama vya Bunge ambavyo havikuunda Serikali. Kiongozi wa upinzani –

- ana cheo baada ya Rais, Naibu Rais, Waziri Mkuu na Spika;
- ana haki ya kushiriki katika hafla zote rasmi;
- ana haki ya kuwa wa pili kujibu, baada ya Waziri Mkuu, kuhusu hotuba ya Rais Bungeni.

Kanuni za Bunge zinahakikisha kuwa Kiongozi wa Upinzani anaweza kutekeleza shughuli zake ipasavyo Bungeni.

***Bunge linavunjwa au linaahirishwa lini?***

Muhula wa Bunge ni miaka mitano kuanzia tarehe ya kikao cha kwanza baada ya uchaguzi. Wakati wowote Jamhuri ikiwa katika vita, muhula wa Bunge unaweza kuongezwa kwa kipindi kisichozidi miezi sita kwa mara moja. Kuongezwa huko ni kwa kura za asilimia sitini na tano za wabunge wote.

Lakini, kuongezwa huko –

- kusizidi miezi kumi na miwili;
- kufanywe kabla ya muhula wa Bunge kumalizika baada ya uchaguzi mkuu.

Bunge linaahirishwa mnamo siku ya thelathini Novemba kila mwaka. Kikao chake huanza mnamo Jumanne ya kwanza ya Februari mwaka unaofuatia.

***Tume ya Huduma ya Bunge***

Majukumu ya Tume ya Huduma ya Bunge ni pamoja na –

- kutoa huduma na vifaa ili kuhakikisha utendakazi bora na thabiti wa shughuli za Bunge;
- kubuni nyadhifa katika huduma za Bunge na kuteua na kusimamia maafisa katika nyadhifa hizo;
- kusimamia makadirio ya fedha za Bunge; na

KATIBA Institute Constitution as an Instrument of Change

- kufanya mambo mengine ili kuendeleza demokrasia ya Bunge nchini na kufanikisha maslahi ya wabunge na wafanyakazi wa Bunge.

## SURA YA KUMI NA MBILI: MAMLAKA YA UTENDAJI

**Sura hii inahusu:**
- **Wale wanaotutawala**
- **Wajibu wao**
- **Wanavyoshika madaraka**

***Rais***

Mamlaka ya utendaji ya Jamhuri ni ya Rais. Hii ina maana kuwa Rais ana mamlaka ya kudhibiti na kuelekeza shughuli za Jamhuri ya Kenya. Rais ni –

- Mkuu wa Taifa;
- Mkuu wa serikali;
- Amiri Jeshi Mkuu wa Vikosi vya Majeshi ya Ulinzi;
- Mwenyekiti wa Baraza la Usalama wa Taifa.

KATIBA Institute
Constitution as an Instrument of Change

***Kuchaguliwa kwa Rais***

Rais anachaguliwa moja kwa moja kwa njia ya siri na wapiga kura waliosajiliwa. Uchaguzi unafanywa kila baada ya miaka mitano, pamoja na uchaguzi wa wabunge, isipokuwa kuwe na nafasi katika kiti cha Rais kabla ya hapo. Rais anachaguliwa kwa muhula usiozidi miaka mitano na anaweza kuchaguliwa tena kwa muhula mmoja zaidi wa mwisho.

***Mgombea wa kiti cha Rais huteuliwaje?***

Mgombea wa kiti cha Rais –

- ana sifa za kuwa mgombea uchaguzi wa Bunge;
- anateuliwa na chama cha kisiasa kilichosajiliwa;
- mgombea wa kujitegemea sharti ateuliwe na wapiga kura elfu kumi (10,000) waliosajiliwa, pamoja na wapiga kura mia moja (100) waliosajiliwa kutoka kila wilaya.

Mtu hawezi kuteuliwa kama mgombea Urais ikiwa –

- anatii taifa la kigeni;
- anafanya kazi au ana wadhifa katika afisi ya umma;

- ni mjumbe wa Tume ya Kikatiba;
- ni mgombea wa uchaguzi wa Bunge; au
- amewahi kuondolewa katika afisi yoyote kwa kwenda kinyume na Katiba au mwenendo mbaya.


***Utaratibu wa Uchaguzi wa Rais***

Ikiwa mgombea mmoja tu ndiye aliyeteuliwa, mgombea huyo anatangazwa kuwa Rais. Ikiwa watu wawili au zaidi wameteuliwa, uchaguzi unafanywa katika kila jimbo la uchaguzi.

Mgombea wa Urais atakayepata zaidi ya asilimia hamsini ya kura zote zilizopigwa kwenye uchaguzi huo na pia amepata asilimia ishirini na tano au zaidi ya kura zilizopigwa katika wilaya nyingi zaidi, atatangazwa mshindi.

Endapo hakuna mgombea aliyechaguliwa, uchaguzi mpya utafanywa. Katika uchaguzi huu mgombea aliyepata idadi kubwa zaidi na mgombea wa pili kupata kura zaidi ndio wagombea pekee.

Mgombea atakayepata kura nyingi zaidi ndiye atakayetangazwa mshindi. Mgombea huyu atatangazwa Rais, lakini, kabla hajaapishwa, anaitwa Rais-Mteule.




KATIBA Institute
Constitution as an Instrument of Change

***Je, masuala kuhusu uhalali wa uchaguzi wa Rais yatasuluhishwa vipi?***

Uchaguzi wa Rais-Mteule unaweza kutolewa malalamiko ikiwa mtu atayawasilisha katika mahakama ya Juu kabla siku saba kumalizika baada ya kutangazwa matokeo ya uchaguzi. Malalamiko yatasikilizwa na yatatolewa uamuzi kabla ya siku saba kumalizika baada ya kuwasilishwa.

***Rais-Mteule anashikaje madaraka?***

Rais-Mteule anaapishwa kabla hajashika madaraka. Anaapishwa Jumanne ya kwanza baada ya siku ishirini na moja kumalizika tangu kutangazwa kwa matokeo ya uchaguzi.

Rais-Mteule atashika wadhifa wake kwa kula na kutii –

- kiapo au tamko la dhati la utiifu; na
- kiapo au tamko la dhati la utekelezaji wa majukumu ya afisi.

Sherehe hufanywa mbele ya Jaji Mkuu au Jaji wa Mahakama ya Juu mnamo tarehe ambapo kipindi cha Rais aliyepo kinamalizika.

***Itakuwaje kama Rais-Mteule akifariki kabla ya kushika madaraka?***

Rais-Mteule akifariki kabla ya kushika madaraka, mtu aliyetangazwa Naibu Rais atashika wadhifa wa Rais na afisi ya Naibu Rais itakuwa wazi. Ikiwa mtu aliyetangazwa Naibu Rais amefariki kabla ya kushika wadhifa wake afisi ya Naibu Rais inatangazwa kwamba iko wazi Rais akishika madaraka. Ikiwa Rais-Mteule na Naibu Rais wamefariki kabla ya kuchukua nyadhifa zao, Spika wa Bunge atashikilia madaraka ya Rais mpaka uchaguzi mpya ufanywe.

***Ni nini majukumu ya Rais?***

Rais ana majukumu kadha ya kitaifa kwa mujibu wa Katiba. Ikiwa Rais hayuko kazini kwa muda au hawezi kutekeleza majukumu ya afisi ya Rais, mtu aliyeshikilia wadhifa wa Rais wakati huo, ana uwezo wa kutekeleza baadhi ya majukumu ya Rais.

Majukumu ya kitaifa ya Rais ni –

- kuhutubia Bunge kila linapofunguliwa, kikao maalum cha Bunge mara moja kwa mwaka, au kuhutubia Bunge wakati wowote;
- kuhutubia taifa kuhusu hatua zilizochukuliwa na maendeleo yaliyofanywa katika kufikia maadili ya taifa, kanuni na malengo;
- kuteua na kufuta maafisa – Waziri Mkuu, Naibu Waziri Mkuu, Mawaziri, Naibu Mawaziri, Majaji, na maafisa wengine wa umma kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa na Katiba;
- kuweka saini mikataba na maafikiano ya kimataifa kama ilivyoidhinishwa na Bunge;
- kutangaza hali ya hatari au vita kama ilivyoidhinishwa na Baraza la Mawaziri;

- kuteua na kupokea wawakilishi wa kidiplomasia (ubalozi) na ukonseli (ubalozi mdogo);
- kuhusiana na uwezo wa kutoa msamaha;
- kutoa tuzo za heshima kwa Wakenya waliohudumia Kenya kwa namna ya kipekee; na
- kuhakikisha kuwa majukumu ya nchi ya kimataifa yanatelekezwa na mawaziri na kila mwaka kuleta taarifa Bungeni kuhusu maendeleo ya utekelezaji wa maafikiano.

Rais ana uwezo, wa kusamehe au kupunguza kifungo cha mtu aliyehukumiwa baada ya kuvunja sheria, akishauriana hivyo na Kamati Shauri ya Uwezo wa Rais wa Kusamehe.

***Rais anaweza kuondolewa vipi madarakani?***

Rais anaweza kuondolewa mamlakani kwa njia mbili –

- kutoweza kazi kwa sababu ya afya ya kimwili au kiakili;
- akitenguliwa – Rais anaweza kuondolewa mamlakani akikiuka masharti ya Katiba hii au akiwa na mwenendo mbaya.

KATIBA
Institute
Constitution as an Instrument of Change

***Kuna utaratibu gani wa kumwondoa Rais kwa ajili ya kutoweza kazi?***

Hatua zifuatazo zinafuatwa katika kumwondoa Rais kwa kutoweza kazi –

- Mbunge anawasilisha hoja Bungeni ya kumwondoa Rais;
- ikiwa hoja imeungwa mkono na angalau nusu ya wabunge, Spika anamfahamisha Jaji Mkuu;
- Jaji Mkuu anateua tume ya afya yenye madaktari watano kabla ya siku saba kumalizika;
- ikiwa Jaji Mkuu hatateua tume hiyo, Spika sharti aiteue kabla siku saba hazijamalizika;
- tume inachunguza hali ya Rais kutoweza kazi na inatoa taarifa kwa Jaji Mkuu au Spika – kutegemea ni nani aliyeiteua – kabla siku kumi na nne hazijamalizika;
- Jaji Mkuu au Spika anaidhinisha taarifa na anachukua hati na taarifa Bungeni; na
- tume ikitoa taarifa kwamba Rais hawezi kutekeleza wadhifa wake na taarifa iidhinishwe na angalau nusu ya wabunge, Rais atatoka mamlakani.

***Ni nini utaratibu wa kumwondoa Rais kwa kumtengua?***

Hatua zifuatazo zinatumika ili kumwondoa Rais kwa kumtengua –

- Mbunge anawasilisha hoja ya kumtengua Rais;

- ikiwa zaidi ya asilimia hamsini ya wabunge wanaiunga mkono hoja hiyo, Bunge linateua kamati maalum ya wanachama kumi na watatu kuchunguza jambo hili;
- kamati maalum inachunguza jambo hili na inatoa taarifa kwa Bunge kabla siku kumi hazijamalizika;
- kamati hii maalum ikitoa taarifa kuwa mashtaka dhidi ya Rais yamethibitishwa, Bunge linapigia kura taarifa; na
- taarifa ikiidhinishwa na asilimia sabini na tano ya wabunge wote, Rais anaondolewa mamlakani.

Afisi ya Rais inaweza kuwa wazi ikiwa Rais –

- amefariki;
- amejiuzulu;
- ameondolewa kutokana na kutoweza kazi kwa ajili ya afya ya mwili au akili;
- ametenguliwa.

***Nafasi ya Rais hujazwa vipi?***

Ikiwa afisi ya Rais iko wazi, Naibu Rais atashika wadhifa wa Rais.

Ikiwa afisi ya Rais na ya Naibu Rais ziko wazi, Spika wa Bunge atashika wadhifa wa Rais.

KATIBA Institute Constitution as an Instrument of Change

***Je, Rais anaweza kushtakiwa mahakamani?***

Mtu aliyeshikilia mamlaka ya Rais hawezi kushtakiwa wakati akiwa mamlakani. Pia, mtu aliyeshikilia mamlaka ya Rais hawezi kushtakiwa wakati akiwa mamlakani kwa kufanya au kutofanya jambo katika kutekeleza nyadhifa alizopewa chini ya Katiba hii.

***Naibu Rais huchaguliwaje?***

Hakutakuwa na uchaguzi wa Naibu Rais. Kabla ya uchaguzi wa Rais, kila mgombea urais atachagua mtu atakayekuwa Naibu Rais, mgombea urais akichaguliwa. Mtu aliyeteuliwa atakuwa na sifa za kuchaguliwa kama Rais.

***Naibu Rais ana muhula gani?***

Muhula wa Naibu Rais utaanza wakati Rais anapochukua madaraka na utamalizika -

- wakati Rais afuataye anapochukua madaraka;
- Naibu Rais anapokuwa Rais; au
- kwa kujiuzulu, kufariki ama kuondolewa madarakani.

Naibu Rais –

- atahudumu kwa muda usiozidi mihula miwili;
- anaweza kujiuzulu kwa kuwasilishia Rais taarifa ya maandishi;
- anaweza kuondolewa kama vile Rais anaweza kuondolewa.

***Itakuwaje afisi ya Naibu Rais ikiwa wazi?***

Ikiwa afisi ya Naibu Rais ni wazi, Rais atamteua mtu aliye na sifa zinazohitajika kwa uchaguzi wa Rais ili achukue wadhifa wa Naibu Rais.

Uteuzi unawasilishiwa Spika kabla siku kumi na nne kumalizika. Bunge linaweza kuidhinisha uteuzi kupitia azimio lililoungwa mkono na thuluthi mbili za wabunge wote. Ikiwa Bunge limetakaa uteuzi kwa mara ya pili, Rais atateua mtu atakayekuwa Naibu Rais.

***Ni nini majukumu ya Naibu Rais***

Naibu Rais –

- ni msaidizi mkuu wa Rais katika kutekeleza majukumu ya Rais;
- anatekeleza majukumu aliyopewa na Katiba hii;
- anatekeleza wajibu kwa niaba ya Rais ikiwa Rais ni mgonjwa au endapo hayupo nchini kwa muda;
- anatekeleza majukumu mengine yoyote anayoweza kupewa na Rais.

***Waziri Mkuu***

Kutakuwa na Waziri Mkuu wa Jamhuri.

***Ni nini majukumu ya Waziri Mkuu?***

Waziri Mkuu anawajibika kwa Rais na katika kufuata maagizo ya Rais –

(a) yeye ni Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni;

(b) anatekeleza majukumu mengine kwa mujibu wa Katiba au kama alivyoagizwa na Rais.

***Waziri Mkuu anateuliwa vipi?***

Waziri Mkuu anateuliwa na Rais kutoka miongoni mwa wabunge.

Utaratibu wa kuteua Waziri Mkuu unaanza kabla ya siku saba kumalizika Bunge likikutana baada ya uchaguzi mkuu au ikihitajika ili kujaza nafasi katika afisi ya Waziri Mkuu. Aliyeteuliwa sharti aungwe mkono na zaidi ya asilimia hamsini ya Wabunge wote. Bunge likikataa kumwunga mkono, Rais atateua mtu mwingine. Bunge likikataa kuidhinisha mteuzi wa pili, Rais anachagua Mbunge kuwa Waziri Mkuu.

***Waziri Mkuu ana mihula mingapi madarakani?***

Muhula wa Waziri Mkuu utaendelea hadi -

- Waziri Mkuu anapofariki,
- Waziri Mkuu anapojiuzulu kwa kuwasilisha taarifa kwa Rais kimaandishi;
- Waziri Mkuu akiondolewa madarakani; au
- mtu mwingine anayeteuliwa Waziri Mkuu baada ya uchaguzi anapochukua madaraka.

***Baraza la Mawaziri***

Baraza la Mawaziri lina Rais, Naibu Rais, Waziri Mkuu, Naibu Waziri Mkuu wawili, Mawaziri, Mwanasheria Mkuu, na Kiranja wa Bunge.

***Je, Manaibu Waziri Mkuu, Mawaziri na Manaibu Mawaziri huteuliwa vipi?***

Manaibu Waziri Mkuu, Mawaziri na Manaibu Mawaziri huteuliwa na Rais.

Manaibu Waziri Mkuu, Mawaziri na Manaibu Mawaziri huteuliwa kutoka miongoni mwa wabunge. Rais ana uwezo wa kuteua mawaziri wasiozidi asilimia ishirini kutoka nje ya Bunge. Wanashika nyadhifa zao kwa kula kiapo na kutii tamko la dhati la afisi zao.

***Muhula wa Manaibu Waziri Mkuu, Mawaziri na Manaibu Mawaziri***

Manaibu Waziri Mkuu, Mawaziri na Manaibu Mawaziri wanaendelea mamlakani hadi –

- kufariki;
- kujiuzulu kwa taarifa ya maandishi – barua za kujiuzulu zinawasilishiwa Waziri Mkuu na Rais;
- wameondolewa kazini; au
- nafasi zao zinachukuliwa na watu wengine baada ya uchaguzi mkuu.

***Ugawaji wa majukumu kwa Baraza la Mawaziri***

Rais anawapa majukumu Naibu Rais, Waziri Mkuu, Naibu Waziri Mkuu, Waziri na Naibu Waziri.

***Baraza la Mawaziri kazini***

Baraza la Mawaziri linawajibika kwa Bunge kama kikundi na kama watu binafsi katika utekelezaji wa majukumu yao. Baraza la Mawaziri linawajibika kwa wizara zao na Mawaziri wanatoa mwelekeo na kudhiti wizara inayohusika. Baraza la Mawaziri litakutana angalau mara moja kwa mwezi. Akidi ya mikutano ya Baraza la Mawaziri itakuwa nusu ya Mawaziri wote.

Uamuzi wa Baraza la Mawaziri utakuwa kwa maandishi na utatiwa sahihi na Rais.

***Katibu wa Baraza la Mawaziri***

Katibu wa Baraza la Mawaziri anateuliwa na kuondolewa madarakani na Rais, baada ya kuidhinishwa na Bunge.

Katibu wa Baraza la Mawaziri –

- ana wadhifa juu ya afisi ya Baraza la Mawaziri;
- anapanga shughuli na kuweka kumbukumbu za Baraza la Mawaziri;
- anawasilisha uamuzi wa Baraza la Mawaziri kwa watu wanaohusika.

***Makatibu Wakuu***

Katibu Mkuu ndiye –

- kiongozi wa kiutawala Wizarani;
- anasimamia shughuli za Wizara kila siku;
- anamshauri waziri kuhusu mambo yote ya Wizara; na
- anateuliwa na Rais na kuidhinishwa na Bunge.

***Mwanasheria Mkuu***

Mwanasheria Mkuu anateuliwa na Rais baada ya kupokea mapendekezo kutoka kwa Tume ya Huduma ya Umma na kuidhinishwa na Bunge.

***Mwanasheria Mkuu ana sifa gani?***

Ili mtu ateuliwe Mwanasheria Mkuu, sharti awe na sifa zinazohitajika kwa uteuzi wa Jaji Mkuu.

***Ni nini wajibu wa Mwanasheria Mkuu?***

Mwanasheria Mkuu ni mshauri mkuu wa serikali katika masuala ya sheria na –

KATIBA Institute Constitution as an Instrument of Change

- anatayarishia Serikali taarifa za kisheria;
- anawakilisha Serikali katika kesi za madai; na
- anarasimu sheria kwa niaba ya serikali.

***Mwanasheria Mkuu ana muhula gani?***

Mwanasheria Mkuu anahudumu kwa muhula wa miaka mitano na anaweza kuteuliwa tena kwa muhula mwingine mmoja wa miaka mitano.

***Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma***

Mkurugenzi wa mashtaka ya Umma anateuliwa na Rais baada ya kupendekezwa na Tume ya Huduma ya Umma na kuidhinishwa na Bunge.

***Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma ana sifa zipi?***

Ili mtu ateuliwe Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma, mtu huyo sharti awe na sifa zinazohitajika kwa uteuzi wa Jaji wa Mahakama Kuu.

***Ni nini majukumu ya Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma?***

Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma anashtaki kesi za uhalifu kwa niaba ya serikali na anaweza –

- kuleta mashtaka ya uhalifu dhidi ya mtu yeyote;
- kutwaa kesi za jinai zilizowasilishwa na watu wengine;
- kwa idhini ya mahakama, kusimamisha kesi yoyote ya uhalifu kabla ya hukumu kutolewa; na
- kuelekeza Inspekta Mkuu wa Polisi ya Kenya kufanya uchunguzi kuhusu uhalifu.

***Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma anahudumu kwa muda gani?***

Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma anahudumu kwa miaka kumi na hawezi kuteuliwa tena.

***Wakili wa Umma***

Wakili wa Umma atateuliwa na Rais baada ya kupokea mapendekezo ya Tume ya Huduma ya Umma na kuidhinishwa na Bunge.

KATIBA Institute
Constitution as an Instrument of Change

***Wakili wa Umma ana sifa gani?***

Mtu anayeteuliwa Wakili wa Umma ana sifa zinazohitajika kwa uteuzi wa Jaji wa Mahakama Kuu.

***Wakili wa Umma ana majukumu gani?***

Wakili wa Umma anatoa ushauri wa kisheria na anawakilisha watu wasioweza kugharamia huduma za kisheria.

***Kuondolewa madarakani kwa Mwanasheria Mkuu, Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma na Wakili wa Umma***

Mwanasheria Mkuu, Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma na Wakili wa Umma anaweza kuondolewa mamlakani ikiwa –

- ameshindwa kutekeleza wadhifa wake kwa sababu ya ugonjwa;
- ameshindwa kufuata kanuni zinazohusu uadilifu kwa mujibu wa Sura ya Tisa ya Katiba hii;
- amefilisika;
- hana ujuzi wa kutosha wa kazi inayohitajika; au
- ana tabia ama mwenendo mbaya.

***Nini utaratibu wa kuondoa Mwanasheria Mkuu, Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma na Wakili wa Umma?***

- Mtu yeyote anaweza kulalamikia Tume ya Huduma ya Umma akitaka Mwanasheria Mkuu, Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma au Wakili wa Umma kuondolewa kazini;
- Tume ya Huduma ya Umma ikitosheka kwamba malalamiko ni halali, itayapelekea Rais;
- baada ya kupokea malalamiko, Rais atamsimamisha kazi Mwanasheria Mkuu, Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma au Wakili wa Umma na kuteua mahakama maalum itakayopendekeza kama inafaa Mwanasheria Mkuu, Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma au Wakili wa Umma kuondolewa mamlakani;
- katika kutoa uamuzi, Rais sharti afuate mapendekezo ya mahakama maalum.

KATIBA Institute Constitution as an Instrument of Change

# SURA YA KUMI NA TATU: MAHAKAMA

**Sura hii inahusu:**
- **Namna sheria zetu zinatekelezwa mahakamani na kwingineko**

***Uwezo wa mahakama***

Uwezo wa mahakama unatokana na watu na utatumiwa na mahakama pamoja na mahakama maalum. Katika kutumia uwezo huu sharti mahakama na mahakama maalum zifuate Katiba na Sheria za Kenya.

***Kanuni zinazoongoza Mahakama na Mahakama Maalum***

Mahakama na mahakama maalum huongozwa na kanuni zifuatazo –

- watu wote watashughulikiwa kwa uadilifu;
- uamuzi utatolewa bila kuchelewa;
- watu waliokosewa sharti walipwe fidia ipasavyo;
- taratibu zinazofuatwa lazima ziwe nyepesi na rahisi kueleweka;
- kutumia mahakama za jadi kutahimizwa.

***Wanachama wa Mahakama ni nani?***

Wanachama wa Mahakama ni –

- majaji;
- mahakimu; maafisa wakuu wasimamizi na maafisa wasimamizi wa mahakama ya dini, Kadhi Mkuu na Kadhi; na
- maafisa wengine wa mahakama.


***Kenya ina mahakama zipi?***

Kenya ina mahakama zifuatazo zilizopangwa kutoka mahakama ya juu hadi ya chini –

- Mahakama ya Juu;
- Mahakama ya Rufani;
- Mahakama Kuu;
- Mahakama za Hakimu, Mahakama za Kikristo, Mahakama za Kadhi, Mahakama za Kihindu, na Mahakama zingine za kidini;
- Mahakama za kijeshi;

KATIBA Institute
Constitution as an Instrument of Change

- Mahakama za kijadi;
- Mahakama maalum zilizoundwa na sheria za Bunge; na
- Mahakama nyingine za chini zilizoundwa na Sheria za Bunge.




***Uhuru wa mahakama***

Mahakama iko huru na haiwajibiki kwa mamlaka yoyote au mtu.

***Jaji Mkuu na Naibu Jaji Mkuu***

Jaji Mkuu ndiye kiongozi wa Mahakama. Jaji Mkuu anabaki mamlakani kwa muda wa miaka kumi au akitimiza miaka sabini.

Naibu Jaji Mkuu ni msaidizi mkuu wa Jaji Mkuu.

***Mahakama ya Juu***

Mahakama ya Juu itakuwa na –

- Jaji Mkuu, ambaye ndiye Rais wa Mahakama;
- Naibu Jaji Mkuu, atakayekuwa Makamu wa Rais wa Mahakama; na
- Majaji wengine wasiopungua watano na wasiozidi saba.

Mahakama ya Juu ndiyo mahakama yenye uwezo wa kuamua kuhusu kesi zifuatazo –

- kesi za uchaguzi wa Urais;
- kesi zinazohusu kutenguliwa kwa Rais; na
- rufaa kutoka Mahakama ya Rufani au kutoka mahakama nyingine au mahakama maalum kama ilivyoagizwa na Sheria.

**Mahakama ya Rufani**

Mahakama ya Rufani ina –

KATIBA Institute Constitution as an Instrument of Change

- Rais wa Mahakama ya Rufani; na
- Majaji wengine.

Inasikiliza rufaa kutokana na uamuzi wa Mahakama Kuu ama Mahakama nyingine au Mahakama Maalum.

***Mahakama Kuu***

Mahakama Kuu ina –

- Jaji Kiongozi; na
- Majaji wengine.

***Mamlaka ya Mahakama Kuu***

Mahakama Kuu ina mamlaka ya kuamua kesi zifuatazo –

- kesi za jinai na za madai;
- masuala yote kuhusu ufafanuzi na utekelezaji wa masharti ya Katiba; na
- kesi nyingine ambazo sheria inaweza kuhitaji zisikilizwe na kuamuliwa.

Mahakama Kuu itakuwa na mamlaka ya usimamizi wa mahakama na mahakama maalum nyingine zilizo chini yake.

***Je, Jaji Mkuu, Naibu Jaji Mkuu, au Majaji wengine huteuliwa vipi?***

Utaratibu wa kuteua Jaji Mkuu, Naibu Jaji Mkuu, au Majaji wengine ni kama ifuatavyo –

- pendekezo linatolewa na Tume ya Huduma ya Mahakama;
- pendekezo linaidhinishwa na Bunge; na
- uteuzi wa mwisho unafanywa na Rais.

***Ni nani anaweza kuwa Jaji Mkuu, Naibu Jaji Mkuu, au Jaji?***

Jaji Mkuu, Naibu Jaji Mkuu, Majaji wa Mahakama ya Juu na wa Mahakama Kuu ni watu ambao –

- wanaelewa vyema sheria na wanaweza kufanya kazi inayohitajika katika nyadhifa hizo; na
- ni watu wenye mwenendo wa uadilifu na uaminifu wa hali ya juu.

***Sifa nyingine za kuteuliwa kuwa jaji***

Pamoja na hayo,

- Jaji Mkuu au Jaji wa Mahakama ya Juu ni mtu mwenye uzoefu wa angalau miaka kumi na mitano nchini Kenya au katika nchi nyingine yenye mfumo wa sheria ya Jumuiya ya Madola kama Jaji wa Mahakama ya Rufani au Mahakama Kuu; au akifanya kazi kama wakili wa umma au binafsi;
- Jaji wa Mahakama ya Rufani ni mtu aliyehudumu kwa miaka kumi na miwili nchini Kenya au katika nchi nyingine yenye mfumo wa sheria ya Jumuiya ya Madola kama Jaji wa Mahakama ya Rufani au Mahakama Kuu, au akifanya kazi kama wakili wa umma au binafsi;
- Jaji wa Mahakama Kuu ni mtu aliyehudumu kwa miaka kumi nchini Kenya au katika nchi nyingine yenye mfumo wa sheria ya Jumuiya ya Madola kama Jaji wa Mahakama ya Rufani au Mahakama Kuu, au akifanya kazi kama wakili wa umma au binafsi.

KATIBA Institute
Constitution as an Instrument of Change

***Majaji wanastaafu lini?***

Jaji anastaafu anapofikia umri wa miaka sabini.

***Jaji anaweza kuondolewa madarakani lini?***

Jaji anaweza kuondolewa madarakani ikiwa –

- ameshindwa kufanya kazi kwa ajili ya ugonjwa;
- amefilisika;
- hana ujuzi wa kutekeleza kazi ipasavyo; au
- ana tabia mbaya au mwenendo mbaya.

***Nini utaratibu wa kumwondoa Jaji madarakani?***

Mtu yeyote anaweza kutoa malalamiko kwa Tume ya Huduma ya Mahakama akiomba Jaji aondolewe madarakani. Ikiwa Tume ya Huduma ya Mahakama imetosheka kwamba malalamiko ni halali, itayapeleka kwa Rais. Baada ya kupokea malalamiko Rais atamsimamisha Jaji kazi na ateue mahakama maalum kukata kauli kama inafaa Jaji aondolewe madarakani. Rais sharti afuate uamuzi wa mahakama maalum.

***Mahakama za Kidini***

Mahakama zifuatazo za kidini zinatambuliwa Katiba –

- Mahakama za Kikristo
- Mahakama za Kadhi; na
- Mahakama za Kihindu.

Bunge lina uwezo wa kuunda mahakama nyingine za kidini.

Mahakama za kidini zinasimamiwa na maafisa wakuu, Kadhi Mkuu, na maafisa wasimamizi au Kadhi wa dini zinazohusika. Bunge linatunga sheria kuhusu namna mahakama za kidini zinavyofanya kazi.

***Mahakama za kidini zinashughulika na kesi zipi?***

Mahakama za kidini zinashughulikia masuala ya sheria za kidini kuhusu hadhi ya binafsi, ndoa, talaka, na urithi. Washirika wote katika mahakama za kidini ni wafuasi wa imani inayohusika.

KATIBA Institute Constitution as an Instrument of Change

***Tume ya Huduma ya Mahakama***

Tume hii ina –

- Jaji Mkuu ambaye ni mwenyekiti;
- Jaji mmoja wa Mahakama ya Juu;
- Jaji mmoja wa Mahakama ya Rufani;
- Jaji mmoja wa Mahakama Kuu;
- Mwanasheria Mkuu;
- mawakili wawili; na
- mtu mmoja aliyeteuliwa na Tume ya Huduma ya Umma.

***Majukumu ya Tume ya Huduma ya Mahakama***

Wadhifa wa Tume ya Huduma ya Mahakama ni pamoja na –

- kuhakikisha na kuendeleza uhuru na uwajibikaji wa mahakama;
- kupendekeza kwa Rais watu wa kuteuliwa kuwa majaji;
- kuteua, kuchukua hatua za kinidhamu na kuwaondoa wasajili, mahakimu na maafisa wengine wa mahakama;
- kutayarisha na kutekeleza mipango ya elimu na mafunzo kwa majaji, mahakimu na maafisa wengine wa mahakama; na
- kuishauri serikali kuhusu kuongeza ufanisi wa mahakama.

## SURA YA KUMI NA NNE: SERIKALI ILIYOSAMBAZWA MAMLAKA

**Sura hii inahusu:**
- **Namna tunavyojitawala katika ngazi ya wilaya**

***Ni nini usambazaji wa madaraka?***

Usambazaji wa mamlaka unahusu namna uwezo wa watu kudhibiti masuala ya nchi na kuamua namna maliasili ya nchi itakavyogawanywa baina ya ngazi mbalimbali za serikali.

Usambazaji wa mamlaka unahitajika ili –

- kutuwezesha kulinda haki zetu za kidemokrasia na kutuwezesha tutekeleze wajibu wetu katika kujitawala;
- kutuwezesha tujitawale kwa uwazi;
- kuwezesha jamii kusimamia mambo yao na kujiendeleza;
- kulinda haki za jamii zilizotengwa;
- kuhakikisha ugawaji ulio sawa wa maliasili kote nchini Kenya; na
- kutuwezesha kufikia huduma za Serikali kote nchini Kenya.

***Serikali ya Wilaya***

Serikali yetu ina ngazi mbili – taifa na wilaya. Sheria inaonyesha namna ngazi hizi zinafanya kazi. Wilaya ndiyo ngazi muhimu zaidi katika usambazaji wa mamlaka.

KATIBA Institute
Constitution as an Instrument of Change

***Ngazi za Serikali iliyosambazwa zinafanya kazi namna gani?***

Katika kutekeleza majukumu yake kila ngazi ya Serikali itahakikisha kuwa haiingilii ngazi nyingine ya Serikali. Kila ngazi ya Serikali lazima iheshimu haki na nafasi ya kikatiba ya ngazi nyingine ya Serikali. Kila ngazi ya Serikali lazima isaidie na iunge mkono ngazi nyingine ya Serikali na iheshimu sheria zake. Kila ngazi ya Serikali lazima itoe taarifa kwa ngazi nyingine ya Serikali na ifanye kazi na ngazi hiyo kuhusu namna ngazi hizi zinaweza kutekeleza wajibu wake kwa njia iliyo bora. Serikali za Wilaya zinaweza kuunda kamati na mamlaka za pamoja ikihitajika ili zifanye kazi kwa pamoja.

Bunge linatunga sheria ili kusaidia Serikali za Wilaya na Serikali ya Taifa kusuluhisha mizozo baina yake.

***Majukumu ya kila ngazi ya Serikali***

Kila ngazi ya Serikali ina wajibu na majukumu.

Majukumu ya Serikali ya Taifa ni –

- mambo ya nchi za Kigeni;
- matumizi ya maji ya kimataifa;
- uhamiaji na uraia;
- ulinzi na usalama wa taifa; na
- mahakama.

KATIBA Institute Constitution as an Instrument of Change

Majukumu ya Serikali ya Wilaya ni –

- kutunga sera za wilaya;
- kilimo wilayani;
- huduma za afya wilayani;
- shughuli za kitamaduni wilayani; na
- usafiri wilayani.


Serikali za Wilaya zinaleta huduma zake karibu nasi kwa kusambaza mamlaka kwa ngazi nyingine za chini, kila inapowezekana, ili zitoe baadhi ya huduma.

Wakati majukumu ya Serikali ya Taifa yanatolewa kwa Serikali ya Wilaya, fedha zitakazowezesha Serikali ya Wilaya kutekeleza majukumu hayo lazima zitolewe.

Katika kutekeleza majukumu yake Serikali ya Taifa na ya Wilaya hupewa fedha na Hazina Kuu ya Taifa. Pia Serikali ya Wilaya inaweza kukusanya fedha kwa kutoza kodi.

*Mgongano wa Sheria za Taifa na za Wilaya*

Serikali ya Taifa na kila Serikali ya Wilaya ina uwezo wa kutunga sheria kuhusu masuala yanayoihusu. Ikiwa kuna mgogoro baina ya sheria ya taifa na sheria ya wilaya, sheria ya taifa itatumika.




*Maeneo ya mijini wilayani*

Sheria za taifa zinaonyesha namna ya kusimamia maeneo ya mijini wilayani.

Sheria za Taifa –

- zinatofautisha baina ya maeneo ya mijini wilayani na maeneo ya mashambani wilayani;
- zinaonyesha namna eneo katika wilaya linaweza kuwa eneo la mjini; na
- zinafafanua namna wenyeji wa maeneo ya mijini wilayani wanaweza kushiriki katika utawala wa wilaya zao.

*Kusimamishwa kwa Serikali ya Wilaya*

Serikali ya Wilaya inaweza kusimamishwa kwa muda usiozidi siku tisini ikiwa –

- kuna vita nchini Kenya;
- tuko vitani na nchi nyingine; ama
- ikiwa Serikali ya Wilaya imeshindwa kufanya kazi au ni fisadi.

Kabla Serikali ya Wilaya haijasimamishwa –

- Tume Huru ya Uchunguzi lazima ichunguze kama mashtaka ni halali au la; na
- Tume ya Uchunguzi iwe imependekeza kwamba Serikali ya Wilaya isimamishwe.

Sheria inaonyesha namna ya kutekeleza kazi ya serikali iliyosimamishwa.

KATIBA Institute Constitution as an Instrument of Change

***Ukumbi wa Kitaifa wa Serikali za Wilaya***

Kuna kikao kinachoitwa Ukumbi wa Kitaifa cha Serikali za Wilaya. Kila Serikali ya Wilaya inawakilishwa katika ukumbi huu. Ukumbi huu unaziwezesha Serikali za Wilaya kupanga kazi zake. Pia inashauriana na Serikali ya Taifa kuhusu masuala ya Serikali za Wilaya.

Katiba inaruhusu Serikali za Wilaya kushirikiana katika kutekeleza majukumu yake. Ili kufanya hivyo, serikali mbalimbali za wilaya zinaweza kuungana na kuunda Ukumbi wa Kitaifa.




***Serikali za Wilaya***

Kila wilaya itakuwa na Serikali ya Wilaya yenye –

- Ukumbi wa Wilaya; na
- Baraza la Wilaya.

Majadiliano ya wajumbe wa wilaya na Baraza la Wilaya lazima yawe wazi kwa umma na waandishi wa habari.

***Kazi ya Ukumbi wa Wilaya ni gani?***

Ukumbi wa Wilaya ndio unatunga Sheria za Serikali ya Wilaya.

***Ni nani wajumbe wa wilaya?***

Wajumbe wa wilaya ni –

- Mwanachama mmoja aliyechaguliwa kutoka kila wodi ya wilaya; na

KATIBA Institute
Constitution as an Instrument of Change

- Wanachama maalum ambao wote ni wanawake. Wanachama maalum wanachaguliwa baada ya uchaguzi wa mwanachama mmoja kutoka kila wodi ya wilaya ili wanawake wawe thuluthi moja ya wanachama wa kila baraza la wilaya;
- Wanachama walioteuliwa na vyama vya kisiasa ili kuwakilisha maslahi maalum.

Wajumbe wa wilaya wanachaguliwa kwa muhula wa miaka mitano.

***Baraza la Wilaya***

Baraza la Wilaya lina –

- Mwenyekiti wa Wilaya aliyechaguliwa;
- Naibu Mwenyekiti wa Wilaya aliyechaguliwa; na
- Wanachama wengine walioteuliwa na mwenyekiti wa wilaya kwa idhini ya wajumbe wa wilaya kutoka miongoni mwa wajumbe hao.

Wanachama wa Baraza la Wilaya lazima wadhihirishe uanuwai wilayani (kwamba wilaya ina watu wa aina mbalimbali).

***Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Wilaya, Naibu Mwenyekiti wa Wilaya na Mihula yao madarakani***

Sheria inaonyesha utaratibu wa uchaguzi wa Mwenyekiti wa Wilaya na Naibu Mwenyekiti wa Wilaya.

KATIBA Institute
Constitution as an Instrument of Change

Mwenyekiti wa Wilaya na Naibu Mwenyekiti wako madarakani kwa muhula mmoja wa miaka mitano na wanaweza kugombea uchaguzi kwa muhula mwingine mmoja.

***Ni nini kazi ya Baraza la Wilaya?***

Baraza la Wilaya linahakikisha kuwa –

- sheria zilizotungwa na wajumbe wa wilaya zinafanya kazi ipasavyo;
- sheria za kitaifa zinafanya kazi ipasavyo wilayani; na
- kazi za ngazi mbalimbali wilayani zinaendelea ipasavyo.

Baraza la Wilaya linaweza pia kutayarisha sheria za kupitishwa na wajumbe wa wilaya na kufanya kazi nyingine walizopewa na sheria za taifa au wilaya.

Wanachama wa Baraza la Wilaya wanawajibika kwa wajumbe wa wilaya kibinafsi na kwa pamoja. Baraza linahitajika kutoa taarifa kwa wajumbe wa wilaya mara kwa mara wakieleza namna wanavyofanya kazi.

***Sheria za Serikali za Wilaya***

Sheria zilizotungwa na Serikali wa Wilaya sharti zichapishwe kwenye Gazeti la Serikali ya Kenya kabla hazijaanza kutekelezwa.

***Utekelezaji wa muundo wa Usambazaji Mamlaka***


Sheria imeonyesha namna Serikali ya Wilaya inavyofanya kazi.

## SURA YA KUMI NA TANO: FEDHA ZA UMMA NA USIMAMIZI WA MAPATO

**Sura hii inahusu:**

- **Namna Serikali yetu inapata fedha**
- **Namna serikali inalinda fedha za umma**

Lengo la mfumo wa fedha za umma na usimamizi wa mapato ni kuhakikisha ufuataji wa kanuni za uwazi na uwajibikaji katika kusimamia fedha za umma. Mfumo huu pia unahakikisha kushiriki kwa walipakodi katika kuamua namna fedha zao zitatumiwa na Serikali.




KATIBA Institute Constitution as an Instrument of Change

***Kutoza kodi***

Fedha za umma hukusanywa kwa kutoza kodi. Kutoza kodi au kubadilisha kodi, ada au malipo yoyote kwa niaba ya Serikali hakuruhusiwi isipokuwa kama sheria imeruhusu kufanya hivyo.

Ngazi zote za Serikali – ya taifa na ya wilaya – zina uwezo tofauti kuhusu utozaji kodi.

***Kugawa fedha za taifa miongoni mwa Serikali za Wilaya***

Serikali sharti iendeleze mfumo unaosawazisha maendeleo katika sehemu zote kwa kuipa kila Serikali ya wilaya fungu sawa la mapato. Mgawo wa fungu kwa Serikali ya taifa na Serikali za wilaya hutegemea hali kama vile tofauti za kimaendeleo baina ya maeneo tofauti na dharura inayoweza kutokea katika sehemu yoyote.

***Mfuko Mkuu wa Fedha za Serikali***

Fedha zote zinazopokewa na Serikali zinalipwa kwa Mfuko Mkuu wa Fedha za Serikali. Fedha hazitatolewa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali isipokuwa kama imeruhusiwa na Katiba hii au sheria nyingine.

***Mfuko wa Mapato ni nini?***

Kuna mfuko unaoitwa Mfuko wa Mapato katika kila Serikali ya wilaya. Pesa zote zinazopokewa na Serikali ya wilaya zinawekwa kwenye mfuko huu. Fedha zinazohitajika kwa kazi ya Serikali ya wilaya zinatoka mfuko huu.

KATIBA Institute
Constitution as an Instrument of Change

***Mfuko wa Dharura***

Kuna mfuko unaoitwa Mfuko wa Dharura. Fedha kutoka Mfuko huu zinatumika pakitokea dharura ambayo haikutarajiwa kwenye bajeti. Bunge litatunga sheria kuhusu matumizi ya fedha za Mfuko wa Dharura.

***Ukopaji wa Serikali***

Serikali inaweza kukopa fedha kutoka chanzo chochote. Kabla ya kukopa, Serikali ya taifa sharti ipate idhini ya Bunge. Serikali ya wilaya inaruhusiwa kukopa fedha kwa idhini ya wajumbe wa wilaya.

Kiasi kitakachokopwa na Serikali ya taifa na ya wilaya hakitazidi asilimia fulani ya rasilmali ya taifa.  Asilimia hii inawekwa na sheria.

Sheria ya Bunge itaweka masharti vile Serikali ya taifa au Serikali ya wilaya itadhamini mikopo.

***Bajeti***

Bajeti zina mapendekezo ya vile Serikali ya taifa au ya wilaya itakusanya na kutumia fedha kila mwaka.  Katika kutayarisha bajeti ya Serikali ya taifa na wilaya, fedha zitatolewa kwa ajili ya maeneo yaliyotengwa pamoja na jamii zilizotengwa.

***Umma unashiriki vipi katika kutengeneza bajeti?***

Wananchi lazima washirikishwe katika kutayarisha bajeti.  Maoni yao na ushauri wa Baraza la Uchumi na Jamii huzingatiwa na Bunge wakati wa kutayarisha bajeti.

***Serikali hununua vipi bidhaa na huduma?***

Ikiwa Serikali inataka kununua bidhaa itafanya hivyo kwa njia ya haki, usawa, uwazi na ushindani.  Sheria inafafanua jambo hili.

***Namna taasisi za umma zitatumia fedha za Serikali***

Fedha za Serikali lazima zitumiwe vyema na kwa kuwajibika.  Katibu Mkuu anayesimamia wizara na maafisa wa uhasibu katika wizara, Idara au Shirika la Umma watawajibika kwa Bunge katika matumizi ya fedha za umma.

Ikiwa fedha za umma zitatumika vibaya, Hazina Kuu itasimamisha uhamishaji wa fedha kwa wizara, idara, au shirika la umma linalohusika.  Hazina Kuu haiwezi kusimamisha uhamishaji wa zaidi ya asilimia hamsini ya fedha ambazo zingepokewa na Serikali ya Wilaya.  Bunge linaweza kuidhinisha au kutoidhinisha hatua hiyo ya Hazina Kuu.

***Msimamizi wa Bajeti na Mkaguzi Mkuu***

Afisi za Msimamizi wa Bejeti na Mkaguzi Mkuu zimeundwa na Katiba. Afisi hizi ni muhimu sana katika kulinda fedha za umma.  Msimamizi wa Bajeti anahakikisha kuwa fedha zinatolewa kwa mujibu wa bajeti.  Mkaguzi Mkuu anahakikisha kuwa fedha zinatumika ipasavyo.

KATIBA Institute
Constitution as an Instrument of Change

***Taasisi Nyingine za Fedha za Umma***

***(a) Mamlaka ya mapato ya Taifa***

Mamlaka ya Mapato ya Taifa ina wajibu wa kukusanya mapato ya Serikali ya Taifa. Sheria inaonyesha muundo, majukumu na shughuli za Mamlaka ya Mapato ya Taifa.

***(b) Tume ya Mgawo wa Mapato***

Wajibu mkuu wa Tume ya Mgawo wa Mapato ni kukata kauli kuhusu msingi wa mgawo wa mapato ya maliasili ya taifa miongoni mwa ngazi mbalimbali za Serikali. Tume pia ina uwezo wa kusuluhisha migogoro baina ya Serikali ya taifa na Serikali za wilaya kuhusu mgawo wa maliasili ya taifa. Wawakilishi wa Serikali za wilaya wanateuliwa kwa Tume hii na Ukumbi wa Taifa wa Serikali za Wilaya.

***(c) Benki Kuu ya Kenya***

Benki Kuu ya Kenya ndiyo mamlaka ya pekee ya kutoa sarafu za Kenya. Inafanya kazi kama benki na pia mshauri wa fedha kwa serikali. Wajibu mkuu wa Benki Kuu ni kuhimiza na kuendeleza maendeleo ya kiuchumi kwa kuhakikisha kuwa kuna mfumo mzuri wa benki nchini.

Benki Kuu iko chini ya Mamlaka ya Halmashauri yenye Gavana, ambaye ni mwenyekiti, Naibu Gavana na wajumbe wengine wasiozidi watano. Wajumbe wote wa Halmashauri hii wanateuliwa na Rais na kuidhinishwa na Bunge. Wanahudumu kwa muhula wa miaka mitano lakini wanaweza kuteuliwa tena kwa muhula mmoja zaidi wa miaka mitano.

***Picha za Sarafu za Kenya***

Noti na sarafu zinaweza kuwa tu na picha ya Rais wa kwanza wa Jamhuri ya Kenya. Picha nyingine zinazoonyesha hali muhimu za Kenya zinaweza kuwekwa kwenye sarafu.




KATIBA Institute
Constitution as an Instrument of Change

*Baraza la Uchumi na Jamii*


Baraza la Uchumi na Jamii limeundwa ili kushauri serikali kuhusu sera nzuri za kiuchumi. Wajumbe wake wanateuliwa na Rais kwa idhini ya Bunge. Wakati wa kuteua wajumbe wa Baraza, juhudi zifanywe ili jamii mbalimbali za Kenya ziwakilishwe.

## SURA YA KUMI NA SITA: UTUMISHI WA UMMA

**Sura hii inahusu:**
- **Kazi ya watumishi wa umma**
- **Maslahi ya watumishi wa umma**
- **Malipo ya watumishi wa umma**

Maadili na kanuni zinazoongoza utumishi wa umma ni pamoja na –

- kudumisha na kuendeleza viwango vya juu vya maadili ya kitaaluma;
- kutoa huduma bora kwa usawa na haki;
- kufanya kazi kwa uwazi na kuwajibika;
- kuwakilisha uanuwai wa jamii za Kenya, watu wenye ulemavu, na jamii ndogo na zilizotengwa katika muundo wa huduma kwa umma katika ngazi zote.




*Tume ya Utumishi wa Umma*

Tume ya Utumishi wa Umma inahakikisha kuwa Utumishi wa Umma unafanya kazi kwa njia bora. Ina uwezo wa kuunda na kufuta afisi. Pia inateua watu watakaochukua madaraka na inaweza kuwaondoa madarakani.

***Ajira katika Serikali za Wilaya***

Serikali za Wilaya zina jukumu la kuajiri, kuteua, kupandisha cheo, kuhamisha na kufuta kazi watu katika utumishi wake wa umma kwa kuzingatia utaratibu uliofafanuliwa na Sheria ya Bunge.

***Kulinda Maafisa wa Umma***

Maafisa wa Umma wamelindwa dhidi ya kubaguliwa au kuadhibiwa kutokana na utekelezaji wa wajibu wao. Hawawezi kuadhibiwa bila kufuata utaratibu wa sheria.

***Tume ya Uajiri wa Walimu***

Tume ya Uajiri wa Walimu ina uwezo wa kusajili, kuajiri, kuhamisha, kupandisha cheo na kufuta kazi walimu.

***Tume ya Huduma ya Afya***

Tume ya Huduma ya Afya ina uwezo wa kusajili, kuajiri na kupandisha cheo na kuhamisha wahudumu wa afya.

***Tume ya Mishahara na Malipo***

Tume ina wajibu wa kuweka na kurekebisha mishahara na marupurupu ya maafisa wote wa Serikali.

***Huduma ya Kenya ya Kurekebisha Tabia***

Huduma ya Kenya ya Kurekebisha Tabia inahakikisha kuwa wafungwa wamewekwa mahali salama na katika hali ya kibinadamu. Inasaidia wafungwa kubadili tabia zao na kuwawezesha kurudia maisha yenye manufaa katika jamii.

Kiongozi wa Huduma ya Kenya ya Kurekebisha Tabia ni Mkurugenzi Mkuu anayeteuliwa na Rais kwa ushauri wa Tume ya Huduma kwa Umma na kwa idhini ya Bunge. Mkurugenzi Mkuu anashika madaraka kwa muhula wa miaka mitano na anaweza kuteuliwa tena kwa muhula mmoja zaidi wa miaka mitano.

KATIBA Institute
Constitution as an Instrument of Change

## SURA YA KUMI NA SABA: USALAMA WA TAIFA

**Sura hii inahusu:**
- **Usalama wa nchi yetu**

***Usalama wa Taifa ni nini?***

Usalama wa Taifa ni kulinda nchi yetu, watu wetu, na mali zetu dhidi ya vitisho vya ndani na nje.

***Vyombo vya Usalama wa Taifa***

Vyombo vya Usalama vya Taifa ni –

- Vikosi vya Majeshi ya Ulinzi wa Kenya;
- Huduma ya Upelelezi ya Taifa;
- Huduma ya Polisi ya Kenya; na
- Huduma ya Polisi wa Utawala.

KATIBA Institute
Constitution as an Instrument of Change

Vyombo vya Usalama wa Taifa viko chini ya mamlaka ya Katiba na Bunge.
Vyombo vya Usalama lazima viheshimu sheria ya Kenya na sheria ya kimataifa, tamaduni zetu mbalimbali na vilinde haki zetu za binadamu katika utekelezaji wa wajibu wake.
Vyombo vya usalama wa taifa vina jukumu la kuweka amani kwenye mipaka.


***Baraza la Usalama wa Taifa***

Kuna Baraza la Usalama wa Taifa. Wajumbe wa Baraza la Usalama wa Taifa ni –

- Rais;
- Naibu Rais;
- Waziri Mkuu;
- Waziri anayehusika na Ulinzi;
- Waziri anayehusika na mambo ya nje;
- Waziri anayehusika na usalama wa ndani; na
- Mwanasheria Mkuu.

Rais anaongoza mikutano ya Baraza na Naibu Rais anaongoza iwapo Rais hayupo. Iwapo Naibu Rais hayupo, Waziri Mkuu anaongoza.

Baraza la Usalama la Taifa linahitajika kusimamia vyombo vya usalama wa taifa na kuvisaidia vifanye kazi pamoja ili Kenya iwe salama. Linatoa taarifa Bungeni kila mwaka kuhusu usalama nchini Kenya. Kwa idhini ya Bunge, linaweza kutuma majeshi ya taifa yaende nchi za kigeni na linaweza pia kuruhusu majeshi ya nchi nyingine kuingia nchini Kenya ili kudumisha amani na kusaidia shughuli nyingine zinazoweza kuleta amani.




*Vikosi vya Majeshi ya Ulinzi*

Vikosi vya Majeshi ya Ulinzi vinajumuisha –

- Jeshi la Kenya la Nchi Kavu;
- Jeshi la Kenya la Anga; na
- Jeshi la Kenya la Wanamaji.

Hakuna mtu anayeruhusiwa kuanzisha kikosi cha kijeshi ama chenye hadhi ya kijeshi isipokuwa kama ilivyoagizwa na Katiba.

KATIBA Institute Constitution as an Instrument of Change



***Baraza la Ulinzi***

Kuna Baraza la Ulinzi lenye wajibu wa jumla wa sera, kudhibiti na usimamizi wa vikosi vya majeshi ya ulinzi wa Kenya.

Baraza la Ulinzi litakuwa na –

- Waziri anayehusika na ulinzi, atakayekuwa mwenyekiti;
- Naibu Waziri anayehusika na ulinzi, atakayekuwa makamu mwenyekiti;
- Mkuu wa vikosi vya majeshi ya ulinzi wa Kenya;
- Kamanda wa Jeshi la Nchi Kavu;
- Kamanda wa Jeshi la Anga;
- Kamanda wa Jeshi la Wanamaji; na
- Katibu Mkuu katika Wizara ya Ulinzi.

***Uamrishaji Jeshini***

Rais, kwa ushauriano wa Baraza la Ulinzi, atateua mkuu wa vikosi vya ulinzi wa Kenya, Kamanda wa Jeshi la Nchi Kavu, Kamanda wa Jeshi la Anga na Kamanda wa Jeshi la Wanamaji. Mkuu wa Vikosi vya Ulinzi wa Kenya na makamanda wote watatu wa majeshi, ambao ni Kamanda wa Jeshi la Nchi Kavu, Kamanda wa Jeshi la Anga, na Kamanda wa Jeshi la Wanamaji, wanaamrisha Vikosi vya Ilinzi wa Kenya. Katika kutekeleza uamrishaji huu, wanawajibika kwa amri ya jumla na mamlaka ya Rais kama Amri Jeshi Mkuu wa Vikosi vya Ulinzi wa Kenya.

KATIBA Institute
Constitution as an Instrument of Change

***Huduma ya Upelelezi ya Taifa***

Huduma ya Upelelezi ya Taifa ina wajibu wa kukusanya na kuwasilisha habari ambazo ni muhimu kwa usalama wa nchi yetu. Katika kutekeleza wajibu wake, Huduma ya Upelelezi lazima iheshimu haki za binadamu na utawala wa sheria. Huduma nyingine za upelelezi haziwezi kuundwa isipokuwa kama imeruhusiwa na sheria.

***Mkurugenzi Mkuu wa Huduma ya Upelelezi ya Taifa***

Mkurugenzi Mkuu wa Huduma ya Upelelezi ya Taifa ndiye anayeongoza Huduma hii. Mkurugenzi Mkuu anateuliwa na Rais kwa idhini ya Bunge na anahudumu kwa jumla ya mihula miwili ya miaka mitano kila muhula. Mkurugenzi Mkuu anaweza kuondolewa madarakani na Rais.

***Baraza la Upelelezi la Taifa***

Baraza la Upelelezi la Taifa linashauri kuhusu masuala yote ya usalama wa taifa, na sera ya upelelezi, utawala na matumizi ya mapato.

Baraza la Upelelezi la Taifa linajumuisha –

- Waziri anayehusika na Baraza la Upelelezi la Taifa, ambaye ndiye mwenyekiti;
- Waziri anayehusika na Mambo ya Nje;
- Waziri anayehusika na Mambo ya Fedha;
- Mwanasheria Mkuu; na
- Kiongozi wa Utumishi wa Umma.

***Huduma ya Polisi ya Kenya***

Huduma ya Polisi ya Kenya inafanya kazi katika ngazi ya serikali ya taifa. Majukumu yake yamepewa utaratibu ili kuzingatia muundo na usambazaji wa mamlaka.

Ni huduma yenye nidhamu na ni ya kitaalamu. Sharti –

- ilinde na iheshimu haki za binadamu;
- itusaidie kuondoa ufisadi;
- ifanye kazi kwa uwazi na uwajibikaji;
- ifanye kazi na jamii zote ili kuhakikisha amani na usalama; na
- idhibiti na isaidie mashirika yote ya usalama ya kibinafsi na yanayohusiana na Serikali ili kuhakikisha usalama na amani nchini Kenya.

KATIBA Institute
Constitution as an Instrument of Change

Utendakazi wa Huduma ya Polisi ya Kenya uko chini ya Tume ya Huduma kwa Umma.

***Inspekta-Jenerali wa Huduma ya Polisi ya Kenya***

Huduma ya Polisi ya Kenya inaongozwa na Inspekta-Jenerali anayeteuliwa na Rais kwa idhini ya Bunge. Anahudumu kwa muhula mmoja wa miaka mitano. Inspekta-Jenerali anaweza kuondolewa madarakani na Rais.

***Huduma ya Polisi wa Utawala***

Kuna Huduma ya Polisi wa Utawala. Huduma ya Polisi ya Utawala inafanya kazi katika ngazi zote mbili za Serikali na wananchi ili kudumisha amani na usalama. Ni tofauti na Huduma ya Polisi ya Kenya.

Hata hivyo, utendakazi wake uko chini ya Tume ya Huduma ya Polisi.

***Kamanda-Jenerali wa Huduma ya Polisi wa Utawala***

Huduma ya Polisi wa Utawala inaongozwa na Kamanda-Jenerali anayeteuliwa na Rais kwa idhini ya Bunge. Anahudumu kwa muhula mmoja wa miaka mitano.

Kamanda-Jenerali anaweza kuondolewa madarakani na Rais.

***Tume ya Huduma ya Polisi***

Tume ya Huduma ya Polisi itakuwa na –

- mtu anayestahiki kuteuliwa Jaji wa Mahakama Kuu;
- afisa wa Huduma ya Polisi ya Kenya wa cheo cha juu, aliyestaafu;
- afisa wa Huduma ya Polisi ya Utawala wa cheo cha juu, aliyestaafu;
- watu watatu waadilifu waliohudumia umma kwa utumishi bora;
- Inspekta-Jenerali wa Huduma ya Polisi ya Kenya;
- Kamanda-Jenerali wa Huduma ya Polisi ya Utawala.

Tume ya Huduma ya Polisi ina majukumu ya –

- kuajiri, kuteua na kupandisha cheo maafisa wa Huduma ya Polisi ya Kenya na Huduma ya Polisi wa Utawala;
- kuendelea kupitia upya masuala ya mishahara na marupurupu ya maafisa wa Huduma ya Polisi ya Kenya na Huduma ya Polisi wa Utawala;
- kuendelea kupitia upya masuala ya viwango au sifa zinazohitajika kwa watumishi wa Huduma ya Polisi ya Kenya na Huduma ya Polisi wa Utawala; na
- kuweka nidhamu miongoni mwa maafisa wa Huduma ya Polisi ya Kenya na Huduma ya Polisi wa Utawala.

KATIBA Institute
Constitution as an Instrument of Change

## SURA YA KUMI NA NANE: TUME ZA KIKATIBA

**Sura hii inahusu:**
- **Tume zilizoundwa na Katiba**

***Tume za Kikatiba ni zipi, na zinaundwa kwa nini?***

Tume zote zilizoundwa chini ya Katiba hii zinaitwa Tume za Kikatiba.
Zinaundwa ili kusaidia Serikali ya taifa kutekeleza kanuni za Katiba. Tume hizi ziko huru na zinawezesha majukumu muhimu yaliyoko kwenye Katiba yatekelezwe bila kuingiliwa na mashirika mengine ya Serikali au watu. Kila Tume ya Kikatiba inatakikana ianzishe matawi wilayani.

***Ni nani anayeweza kuwa mjumbe wa Tume ya Kikatiba?***

Tume ya Kikatiba lazima iwe na wajumbe wasiopungua watatu na wasiozidi tisa. Wajumbe sharti wawe na sifa zinazohitajika na wachaguliwe kutoka kwenye makundi na jamii zote nchini mwetu. Wanaidhinishwa na Bunge kabla ya kuteuliwa na Rais. Mjumbe anahudumia kwa muhula wa miaka mitano na anaweza kuteuliwa tena kwa muhula mwingine mmoja wa miaka mitano.

Tume ya Kikatiba ina uwezo wa kupokea malalamiko kutoka kwa wananchi. Tume hiyo inaweza kuchunguza malalamiko na inasuluhisha matatizo ili kupatanisha watu. Tume inaweza kutoza faini na pia kuamuru yeyote aliyekosewa alipwe fidia.

***Tume ya Kikatiba inatoa wafanyakazi wapi?***

Tume ya kikatiba inaajiri wafanyakazi wake.

***Mjumbe wa Tume ya Kikatiba anaondolewaje afisini?***

Mjumbe wa Tume ya Kikatiba anaweza kuondolewa kutoka afisi na Rais ikiwa –

- hawezi kutekeleza wajibu wa kazi yake kutokana na ugonjwa wa kimwili au kiakili;
- ana utovu wa nidhamu;
- anatumia vibaya mamlaka ya afisi yake au anaenda kinyume na kanuni za uongozi na uadilifu;
- amefilisika; au

KATIBA Institute
Constitution as an Instrument of Change

- ameshindwa kuimudu kazi inayohitajika.

Rais anateua mahakama maalum ambayo itachunguza mashtaka. Mjumbe anaondolewa madarakani ikiwa mahakama maalum imependekeza hivyo.

***Fedha za Tume***

Tume za Kikatiba zinafanya kazi kwa kutumia fedha kutoka kwa Mfuko wa Fedha za Serikali. Bunge pia linaweza kuidhinisha matumizi ya fedha. Tena Tume inaweza kupokea misaada. Fedha hizi zinakaguliwa na Mkaguzi Mkuu.

***Taarifa za Tume za Kikatiba***

Tume ya Kikatiba sharti iwasilishe taarifa kila mwaka kwa Rais na Bunge kuhusu shughuli zake. Bunge linaweza, wakati wowote, kuiomba Tume ya Kikatiba kuipelekea taarifa kuhusu shughuli zake.




***Je, kuna Tume nyingine?***

Bunge lina uwezo wa kuunda Tume nyingine. Hii ni pamoja na zile zilizoundwa na Katiba.

KATIBA Institute
Constitution as Instrument of Change

## SURA YA KUMI NA TISA: MAREKEBISHO YA KATIBA

**Sura hii inahusu:**
- **Kubadilisha Katiba yetu**




***Katiba inaweza kurekebishwa?***

Katiba yaweza kurekebishwa kupitia njia zilizofafanuliwa hapa chini.

***Kurekebisha sehemu zilizolindwa mahsusi na Katiba***

Katiba ina mahitaji maalum ambayo sharti yatekelezwe kabla sehemu fulani hazibadilishwa. Sehemu hizi zimelindwa mahsusi kwa kufanywa ziwe ngumu kugeuza kuliko sehemu nyingine. Kanuni hizi zinahusu –

- ukuu wa Katiba;
- mipaka ya Kenya;
- mamlaka ya wananchi;
- kanuni na maadili ya Jamhuri;
- Sheria ya Haki za Binadamu;
- muda wa kushika Urais;
- uhuru wa Idara ya Mahakama na Tume za Kikatiba;
- majukumu ya Bunge; au
- utawala wa wananchi katika ngazi zote mbili za Serikali.

KATIBA Institute
Constitution as an Instrument of Change

Kabla marekebisho hayajafanywa kuhusu kanuni hizi, wananchi sharti waidhinishe marekebisho hayo.

***Marekebisho ya sehemu nyingine za Katiba hufanywaje?***

Sehemu nyingine za Katiba zinaweza kurekebishwa na Bunge kupitia utaratibu wake maalum.

***Wananchi wanaweza kurekebisha Katiba kwa njia gani?***

Ikiwa wapiga kura milioni moja waliosajiliwa watapendekeza rekebisho lifanywe kwenye Katiba, na rekebisho hilo liungwe mkono kwa wingi wa kura na wajumbe wa wilaya, Katiba inaweza kurekebishwa ikiwa bunge pia litaidhinisha rekebisho hilo. Hii inaitwa juhudi ya wananchi.

Ikiwa Bunge halitaidhinisha rekebisho, wananchi wanaweza kurekebisha Katiba kupitia kura ya maoni, ikiwa wanakubaliana na rekebisho.

## SURA YA ISHIRINI: MASHARTI YA JUMLA

**Sura hii inahusu:**

- **Mambo ya jumla na maelezo ya maneno yaliyoko kwenye Katiba**

***Ni nini madhumuni ya masharti ya jumla kwenye Katiba?***

Wakati wa kuandika Katiba au sheria nyingine maneno mahsusi wakati mwingine hutumika au kufafanua maana. Kwa hivyo inakuwa muhimu kueleza maneno au vifungu vinavyohusika. Haya ndiyo madhumuni ya masharti ya jumla katika Katiba hii.

***Utekelezaji wa Katiba***

Sehemu zote za Katiba hii zieleweke na zitumike kama vile Sheria ya Haki za Binadamu inaeleweka na kutumika mahakamani au na Tume ya Haki za Binadamu na Haki za Kiutawala.

KATIBA Institute Constitution as an Instrument of Change

***Kuelewa Katiba***

Katiba hii ieleweke na itumike kwa njia ambayo inaendeleza maslahi ya watu wa Kenya. Ikiwa pana mgongano baina ya matoleo ya lugha mbalimbali ya Katiba hii, toleo la Kiingereza litatumika.

***Ufafanuzi***

Kuna ufafanuzi wa baadhi ya maneno na vifungu vilivyotumika katika Katiba.




KATIBA Institute
Constitution as an Instrument of Change

## SURA YA ISHIRINI NA MOJA: MASHARTI YA AKIBA, MPITO NA YANAYOTOKANA NA KUIDHINISHWA KATIBA HII

**Sura hii inahusu:**
- **Utaratibu wa kutoka kwenye Katiba iliyopo hadi Katiba Mpya**

***Ni nini madhumuni ya Sura hii***

Masharti ya mpito na yanayotokana na kuidhinishwa Katiba hii yanaeleza yale yanayotokea wakati Katiba iliyopo inaacha kutumika na Katiba hii inaanza kutekelezwa.




Katiba inasema kwamba Bunge sharti litunge sheria. Sheria hizo hazina budi kutungwa kabla ya tarehe ya mwisho iliyotolewa na Katiba. Ikiwa pana sababu ya kutosha ya tarehe hiyo ya mwisho kutotimizwa, bunge linaweza kuongeza muda usiozidi mwaka mmoja, kwa wingi wa kura ya thuluthi mbili ya wabunge wote.

KATIBA Institute
Constitution as an Instrument of Change

Mwanasheria Mkuu, kwa kushauriana na Tume ya Utekelezaji wa Katiba, atatunga Miswada ili kuwezesha Bunge kupitisha sheria kufikia tarehe ya mwisho inayohitajika. Tarehe ya mwisho ikifika na Bunge lishindwe kupitisha sheria, Miswada hiyo itakuwa sheria mara moja.

Katiba hii itaanza kutekelezwa tarehe itakapoidhinishwa na Rais. Siku hiyo, Katiba iliyopo kabla ya utekelezaji wa Katiba hii, itaacha kutumika.

***Masharti ya Mpito***

Tarehe Katiba mpya itakapoanza kutekelezwa –

- serikali itabaki vivyo hivyo, na sheria zote ambazo hazina mgongano na Katiba mpya zitaendelea kutumika;
- Bunge litaendelea kufanya kazi kwa muda uliobakia wa muhula wake;

- ikiwa uchaguzi mdogo utafanywa, utafanywa chini ya Katiba hii mpya;
- viongozi wa mashinani na madiwani wataendelea kuwa afisini mpaka mipango mipya chini ya Katiba hii ianze kutumika;
- vyama vya kisiasa vitaendelea kuwepo, lakini lazima vitii sheria mpya;
- Rais na Makamu wa Rais wataendelea kushika afisi zao lakini kama Rais na Naibu Rais chini ya Katiba hii mpya;
- Baraza la Mawaziri litabaki kama Baraza la Mawaziri;
- Waziri Mkuu hatateuliwa hadi uchaguzi mkuu ujao;
- utawala wa mikoa utavunjwa na maafisa wa umma wanaohudumia mfumo huo wa utawala watapewa maelekezo mapya;
- watu wote wenye madaraka chini ya Katiba iliyopo wataendelea kuwa madarakani kama kwamba wameteuliwa chini ya Katiba hii;
- kesi zote zilizoko mahakamani zitaendelea;
- Tume zote za Kikatiba zitaundwa kabla miezi kumi na miwili kumalizika;
- Tume ya Utekelezaji wa Katiba itateuliwa ili ifanye kazi kwa miaka mitano au zaidi;
- Bunge lina miezi sita kutunga sheria itakayoipa Tume ya Haki za Binadamu na Haki za Kiutawala uwezo wa kuchunguza na kusuluhisha ukiukaji wa zamani wa haki za binadamu;
- Serikali kupitia matawi yake mbalimbali itafundisha wananchi kuhusu Katiba hii mpya kwa Kiswahili, Kiingereza na lugha za kiasili;
- noti na sarafu zilizoko zitaendelea kutumika;
- wilaya zilizoko zitaendelea kuweko kama wilaya chini ya Katiba mpya hadi zibadilishwe na sheria ya Bunge; na
- sheria ya Bunge itatoa mwelekeo kuhusu namna serikali za Wilaya zitaanza kutekeleza majukumu yake mapya.

KATIBA Institute
Constitution as an Instrument of Change